# Njia ya KURUDI MADHABAHUNI

## JINSI YA KUISHI KILA SIKU KAMA MWANAFUNZI WA YESU



# Njia ya Kurudi Madhabahuni

Jinsi ya Kuishi Kila Siku Kama Mwanafunzi wa Yesu

"Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6).

Mchangiaji Mkuu: Don MacLafferty

Limesahihishwa, kuboreshwa, na kuchapishwa upya kwa ruhusa kwa ajili ya mpango wa Kurudi Madhabahuni.

Hakimiliki 2023, Chama cha Wachungaji cha  Konferensi Kuu

Hakimiliki ya awali 2021 na Don MacLafferty, Katika Uanafunzi.

Msanifu wa Jarada na Kendra Miranda

Shukurani maalumu kwa Melody Mason kwa kuyahariri masomo haya kwa ajili ya matumizi binafsi.

Shukurani pia kwa Lynne Macias na Kendra Miranda kwa kuomba wakati wa kuhariri ili ya yaeleweke kwa ajili ya kuwasilisha kanuni hizi zinazobadili maisha za kumfuata Yesu kama Rafiki, Mwokozi, na Bwana.

Maandiko yamechukuliwa kutoka BIBLIA
Maandiko Matakatifu, 1952 Union Version.

# YALIYOMO

Utangulizi kwa Njia ya Kurudi madhabahuni. ............................ 1
Maelezo kwa Viongozi wa Wanafunzi: Jinsi ya Ku tumia Kitabu Hiki. ..........................................................................3

Mwanafunzi wa Yesu ni nini? ........................................................ 5

Kanuni 1 – Njoo kwa Yesu Kama Ulivyo. .................................... 9
Kanuni 2 – Mheshimu Yesu Kama Bwana .................................18
Kanuni 3 – Mgundue Yesu katika Neno Lake na Maombi.....29
Kanuni 4 – Pata Ubatizo Mpya wa Roho Mtakatifu. ................38
Kanuni 5 – Penda Familia Yako Kwa Kujitoa Mhanga.............45
Kanuni 6 – Wafanye Wengine Wanafunzi wa Yesu .................56
Kanuni 7 – Ishi Utume Uliopewa na Mungu..............................66

Vipi Ukiishi Kama Mwanafunzi wa Yesu?. .................................73
Kiambatanisho 1 – Usiku wa Maombi.........................................76
Kiambatanisho 2 – Jinsi ya Kutoa Ushuhuda Wako................78
Kiambatanisho 3 – Mawazo kwa ajili ya Ibada za Familia.....80
Kiambatanisho 4 – Kugundua Utume Uliopewa na Mungu..88
Kiambatanisho 5 – Vidokezo kwa Ajili ya Tabia Njema za Kidijitali..................................................................................91
Kiambatanisho 6 – Vigezo kwa Ajili ya Kukuza Wanafunzi Wenye Afya...........................................................................93
Kiambatanisho 7 – Funguo za Kupata Uzoefu wa Neno la Mungu.......................................................................................97
Zana za Uanafunzi na Kurudi Madhabahuni...........................100

Utangulizi kwa

# Njia ya Kurudi Madhabahuni

"Kisha Eliya akawaambia watu wote, Nikaribieni mimi. Watu wote wakamkaribia. Akaitengeneza madhabahu ya Bwana iliyovunjika" (1 Wafalme 18:30).

Rafiki mpendwa,

Unatamani kuishi kila siku kama mwanafunzi wa Yesu Kristo?

Ni kilio na maombi yetu ya moyoni kuwa Roho Mtakatifu akuwezeshe kuwasha upya moto na shauku yako binafsi kwa ajili ya kuifanya ibada yako kwa Yesu Kristo iwe kiini cha maisha yako unapoishi kila wakati kama mwanafunzi Wake! Yesu ni Njia ya kurudi madhabahuni na katika kiti cha enzi cha Mungu.

Tunaomba kuwa kijitabu hiki, pamoja na shughuli zake sahili na chagamoto zake za moyoni, siyo tu kuwa kikuvute wewe binafsi karibu zaidi na Yesu bali pia kikupe zana halisi za kuiongoza familia yako, kanisa lako, na marafiki na majirani zako wawe kila siku wanafunzi wa Yesu wanaoishi madhabahuni.

Ellen White aliandika yafuatayo miaka ya mwanzoni mwa 1900; ni maneno sahihi kabisa katika nyakati tunazoishi:

> Nguvu ambayo haijawahi kuonekana kamwe kabla ilionekana ikiugubika ulimwengu. Katika vichekesho, utafutaji wa pesa, katika mashindano ya kupata madaraka, katika kila pambano kwa ajili ya uhai, kuna nguvu ya kutisha inayogubika mwili na akili na roho. Katikati ya mbio hizi zinazotia wazimu, Mungu anasema. Anatuagiza tujitenga na kuwasiliana Naye. "Tulieni, na mjue kuwa Mimi ni Mungu." Zaburi 46:10.

> Wengi, hata katika nyakati zao za aombi, hushindwa kupokea mbaraka wa mawasiliano ya kweli na Mungu. Wakiwa na mizigo yao hurudi katika kazi yao.
>
> Watendakazi hawa kamwe hawapati mafanikio ya juu hadi watakapojifunza siri ya nguvu. Wanapaswa kujipatia wenyewe muda wa kufikiria, kuomba, kumngoja Mungu kwa ajili ya nguvu za kimwili, za kiakili, na za kiroho. Wanahitaji mvuto unaokweza wa Roho Wake.
>
> Wakipokea mvuto huu, watahuishwa kwa uhai mpya. Mwili uliolegea na akili iliyochoka vitaburudishwa,moyo wenye mzigo utapumzishwa. Siyo pumziko fupi katika uwepo Wake, bali mshikamano binafsi na Kristo, kukaa katika ushirika Naye—hili ndilo hitaji letu (Education, uk. 260).

Hili ndilo litakalotokea tunapotumia muda wa kutosha kila siku katika ibada. Yesu anasubiri kukutana nawe. Je, uko tayari kukutana Naye na kujifunza upya maana ya kuwa mwanafunzi Wake, kuishi kila siku madhabahuni?

Ungana nasi katika safari hii yenye sehemu saba za kumfuata Yesu, Njia ya Kurudi Madhabahuni.

<u>Timu ya Konferensi Kuu ya Kurudi Madhabahuni</u>

| | |
|---|---|
| Ramon J. Canals | Jonathan Walter |
| Dwain Esmond | John Feezer |
| Don MacLafferty | Melody Mason Pavel Goia |

Maelezo kwa Viongozi wa Wafuasi

# Jinsi ya Kutumia Kitabu Hiki

Kitabu hiki kimesanifiwa kiwe zana ya kufundishia uamsho, kwa ajili yako binafsi na kwa ajili ya wale ambao Mungu anawaita kuwaongoza katika Njia ya Kurudi Madhabahuni.

Tunajumuisha mawazo machache kwa ajili ya uvuvio binafsi mwanzoni mwa kila sehemu, yakifuatiwa na njia za kina na ushirikishwaji za kufundisha kanuni saba za Kurudi Madhabahuni za kuwa mwanafunzi wa Yesu.

Zana hizi za kufundishia zinaweza kutumika kwa ajili ya ukuaji na/au kwa ajili ya vikundi vidogo vidogo.

Yesu anasema, ", enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi..." (Mathayo 28:19).

Katika kitabu chote, kila kanuni hutumia muundo ufuatao kwa ajili ya kufundishia. Unapofundisha makundi madogo, tunakutia moyo uende moja kwa moja katika sehemu ya Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo kama kilivyoandikwa hapa chini. Uwe unaongoza kikundi kimoja kidogo au unashughulikia vikundi vidogo vidogo vingi kwa pamoja, fuata muundo huo huo. Kwa njia hiyo, kikundi au vikundi hujihusisha na huwa hai tangu mwanzo.

~~Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo~~

JALI

- Swali limetolewa kusaidia kukuza uhusiano na urafiki ndani ya kikundi kidogo na kusaidia wanakikundi kuelewa mahitaji ya kila mmoja.
- Fursa ya uwajibikaji imetolewa kwa ajili ya wahusika kusimulia jinsi Mungu alivyowasaidia kutumia changamoto ya somo lililopita.

UNGANISHA

- Shughuli sahili ya pamoja imetolewa ambayo inaweza

kukisaidia kikundi kuandaa mioyo yao kwa ajili ya neno la Mungu lililoandikwa (Mtumiaji: Shughuli inapaswa kuwa ya kiubunifu ili kulifanya somo lijalo lieleweke kirahisi). Hili huwa daraja kuelekea ukweli wa Biblia utakaofundishwa katika somo lijalo. (Mtumiaji: Kila mwana kikundi anaweza kuomba ombi fupi na sahili linalogusa hitaji moja kwa moja).

- Maelezo ya haraka kuhusu kilichojifunzwa kutokana na shughuli yanaweza kujumuishwa (Mtumiaji: Kila mwana kikundi aeleze alivyomwona Kristo katika somo).

Kabla ya kuanza kujifunza kwa kina, utangulizi kwa kusudi la somo uanafunzi na Kurudi Madhabahuni litatolewa. (Mtumiaji: Wanakikundi wote wanaweza kuomba maombi mafupi yanayogusa mahitaji moja kwa moja).

GUNDUA

- Daima tunaanza kwa ombi, kumwabudu Mungu na kumwuliza Roho Mtakatifu afundishe Neno.
- Ndipo tunaanza kiini cha kila somo: uchunguzi wa Neno la Mungu kumjua Yesu Kristo na kuelewa maana ya kuishi madhabahuni katika uhusiano Naye.

JIZOEZE

- Fursa ya kujizoeza kutumia na kufanyia kazi kilichojifunzwa katika Neno la Mungu itatolewa.
- Kutakuwa na muda wa kutafuta baraka za Mungu kaitka maombi kikundi kinapojiweka wakfu kuufuta ukweli uliogunduliwa.

## CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI

- Hatimaye, kazi ya kufanya na changamoto ya kwenda nayo, inayotokana na kanuni iliyojifunzwa, itatolewa kwa wanakikundi na kwenda nayo nyumbani. Changamoto hii inakusudiwa kuwasaidia wana kikundi kukuza uhusiano na Yesu na kuwapa changamoto kuishi kila siku madhabahuni katika matumizi ya maisha halisi.

Ikiwa unatumia kitendea hiki kuongozea vikundi vingi vidogo vidogo, gawanya kila kikundi katika watu wasiozidi sita kwa kila kikundi. Kama kiongozi, unaweza kuwasilisha kwa

vikundi vingi vidogo vidogo, kimoja baada ya kingine, kwa kadiri ya mahitaji. Ikiwezekana, ni vizuri kuwa na wanafunzi wengine (ambao tayari wameshajifunza kanuni za Njia ya Kurudi Madhabahuni, ulizo nazo katika mikono yako) wasaidie kuwezesha kila kikundi kidogo.

Kama kiongozi, jiweke wakfu kufundisha kile tu ambacho unakiishi kwa neema ya Bwana Yesu. Kwa maneno mengine, ikiwa hukiishi, usikifundishe. Sasa, sisi sote tumevunjika, watu wasio wakamilifu—wenye dhambi wanaomhitaji Mwokozi—kwa hiyo usisubiri mpaka uiishi kila kanuni kikamilifu kabla ya kufundisha kanuni hizi. Badala yake, ziweke kanuni hizi katika mazoezi ya maisha yako ya kila siku sasa na ndipo ufundishe kutokana na safari yako inayoendelea ya kutembea, kuongea, na kumtangaza Yesu. Uwe halisi katika safari yako ya uongozi. Kamwe usiongoze kama mtu ambaye ameshafika kiroho; ongoza kama mtu ambaye bado anaendelea kukua katika safari yako ya Kurudi Madhabahuni.

Pale unapoweza, toa shuhuda zako binafsi. Wanakikundi watakuwa na mwitikio mkubwa zaidi kwa unyenyekevu na hita lako la msaada kuliko kuonesha mwonekano wa ukamilifu.

Ikiwa hujisikii kutofaa kuongoza au kufundisha kanuni hizi, hilo ni jambo jema, kwa sababu upo mahali pakamilifu kwa ajili ya Roho Mtakatifu kufanya kazi kubwa sana kupitia kwako! (Ikiwa unahitaji msaada wa kuandika ushuhuda wako binafsi, tazama Kiambanisho 2.)

Je, uko tayari? Hebu tuanze!

## Mwanafunzi wa Yesu ni nini?

Unaweza kuwa unajiuliza, "Mwanafunzi wa Yesu ni nini?" Neno la Mungu lililoandikwa hujibu swali hili.

Tafadhali omba unapochunguza aya hizi za Biblia kuona aya zingine unazozigundua kwa msaada wa Roho Mtakatifu kuhusu mada hii.

Mwanafunzi wa Yesu...

Mathayo 4:18–20

- Anaenda popote pale Yesu anapoongoza
- Anamtumaini Yesu awe Kamanda na Bwana wake
- Anaachana na chochote kile kinachoziba njia ya kumfuata
- Hudumisha uhusiano mzuri Naye
- Hutamani kuwa kama Yeye katika kila hali
- Anajifunza kutoka Kwake ili awe mvuvi wa watu

Yohana 8:31, 32

- Huendelea katika Neno la Yesu
- Anajua Ukweli
- Anakuwa na uhuru katika Ukweli

Yohana 13:35

- Anawapenda wengine

Yohana 15:7, 8

- Huzaa matunda sana
- Hukaa katika Yesu

Mathayo 16:24

- Hujikana nafsi na kumweka Yesu juu ya kile anachokitaka
- Hubeba msalaba
- Yuko tayari kuteseka ili awe mkweli kwa Yesu

Mathayo 28:19, 20

- Anakwenda kufanya mataifa yote kuwa wanafunzi
- Anabatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu.
- Anafundisha wanafunzi wengine kuzitii amri zote za Yesu

Matendo 1:5, 8

- Anabatizwa na Roho Mtakatifu
- Ni shahidi mwaminifu kila mahali

Swali ambalo sisi sote tunaweza kumwuliza Mungu ni, "Je, kwa sasa naishi kama mwanafunzi wa Yesu?"

Kidogezo cha Kiongozi
Ikiwa unaongoza kikundi kidogo au vidogo, alika kila mwanakikundi afanye utafiti usiotaja jina ufuatao kabla ya kuanza kujifunza. Gawa kalamu na karatasi, ukiwapa fursa kila mwana kikundi kujua kuwa watahitaji kujibu ndiyo au hapana kwa kila swali. Soma maswali kwa sauti kubwa, ukimpa kila mtu kuandika jibu lao la ndiyo/hapana. Baadaye, kusanya karatasi, jumlisha majibu ya ndiyo/hapana kwa kila swali, waeleze wanakikundi matokeo.

Maswali ya Uanafunzi kwa Utafiti Usiotaja Jina (Jibu Ndiyo au Hapana)

1. Una kiu ya jambo jingine zaidi kwa Yesu kuliko mambo uliyonayo kwa sasa?
2. Una amani kuhusu wokovu wako kwa neema kwa njia ya imani?
3. Una muda wa kutosha kila siku, usio na haraka pamoja na Mungu katika Neno Lake lililoandikwa?
4. Una muda wa kutosha kila siku, usio na haraka pamoj na Mungu katika Maombi?
5. Unajisalimisha kila siku kwa Yesu kama Bwana wa nafsi yako yote na wa vyote ulivyonavyo, ikiwa ni pamoja na mtazamo wako na vifaa vyako vya elektroniki?
6. Unaomba na kupokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu kila siku?
7. Unaipenda familia yako kwa kujitoa mhanga?
8. Ukiwa nyumbani, unakuwa na ibada ya familia pamoja na mwenzi na/au watoto wako?
9. Uko huru dhidi ya kitu chochote ambacho kinaweza kukufanya kuwa mtumwa (uchungu, uraibu, vifaa vya kielektroniki, ponografia, uchu, n.k.)?
10. Je, kwa sasa unafanya mtu fulani kuwa mwanafunzi nje ya familia ya kanisa lako kuamini, kufuata na kumshuhudia Yesu?

Matokeo yanafungua macho na kutetemesha.

Unapomaliza kuongea, mwombe mtu yeyote atumie muda mfupi kuomba na kumsihi Roho Mtakatifu kile anachotaka kuwaambia kuhusu matokeo.

Baada ya ombi hili, omba kuwa Roho Mtakatifu aandae kila moyo kupokea na kuishi kanuni saba za Kurudi Madhabahuni za kuishi kila siku kama mwanafunzi wa Yesu.

> "Bwana anaweza kufanya zaidi katika saa moja kuliko tunavyoweza kufanya katika maisha yote, na wakati anapoona kuwa watu Wake wamejiweka wakfu kikamilifu, hebu nikuambie kazi kubwa itafanywa katika muda mfupi, na ujumbe wa ukweli utapelekwa sehemu zenye giza za dunia, haujatangazwa kamwe" (Sermons and Talks, vol. 1, uk. 306.5).

Kila Siku...

# Njoo kwa Yesu Jinsi Ulivyo

Je, nyakati zingine unajisikia kuhitaji kuwa katika hali fulani kabla ya kuja kwa Yesu? Pengine unafikiri ni lazima uwe chanya, mwenye furaha, mwajibikaji, au uwe msafi kimwili na kiakili. Pengine unafikiri ni lazima ujisikie kuwa mtu wa kiroho na kuwa na maisha yaliyopangiliwa kabla ya Yesu hajakupokea.

Katika maneno ya Uvivio, tusome:

> Unapokuja kwa Yesu sasa, kwa unyenyekevu wa moyo, atakupokea kama ulivyo, mwenye dhambi na mchafu. Ataziondoa dhambi zako, Atakupatia haki Yake. Unapaswa kumtarajia, na kumwamini kama Mwokozi wako binafsi, Mwanakondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu. Njoo kwa Yesu kwa imani, kwa usahili wa mtoto. Jisalimishe kikamilifu, na una Neno Lake, "Ye yote ajaye kwangu sitamtupa nje kamwe." Yohana 6:37. Katika kumpokea Kristo kwa imani ya kweli, unapata mbingu yote kwa zawadi hii kubwa (Letters and Manuscripts, Letter 29, 1893, vol. 8, par. 5).

Katika somo hili tutachunguza nini maana hasa ya kuja kwa Yesu kama tulivyo, bila kubadili kitu chochote kwanza.

Omba: Unapoanza kusoma na kujifunza (au kujiandaa kufundisha) hii kanuni ya kwanza ya Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu akufundishe Neno la Mungu katika njia mpya na inayoeleweka! Na mwombe achukue ujumbe kutoka katika Neno Lake na kuuzamisha katika kina cha moyo wako na roho yako—katika kina kirefu kiasi ambacho hutabaki kuwa mtu yule yule.

JALI

1. Mwulize mtu mmoja mmoja kwa zamu aseme neno moja linaloelezea vizuri siku yake hadi hapo. Sikiliza kwa makini: sherehekea mambo mazuri na onesha huruma kwa yale yasiokuwa mazuri sana.
2. Mwisho wa somo hili, tutakupa changamoto ya kufanya kila siku. Tutakapokutana tena, kile ambacho Mungu alitusaidia kukifanya kupitia changamoto ya somo hili. Kila somo litakuwa na changamoto mpya.

UNGANISHA

1. Kila mtu anamgeukia mwenzake katika kikundi na kumweleza mambo mawili anayoyafanya anapojua kuwa wageni wanakuja katika nyumba yake.
2. Je, baadhi yenu mnaweza kutueleza jinsi mnavyojiandaa kwa ajili ya kuwa na mtu mwingine? (Ruhusu mjadala wa wazi.)
3. Vipi kama Yesu angekuja katika nyumba yako? Je, unajiskia kuwa unahitaji uwe katika hali fulani kabla ya kumfungulia mlango au kabla ya kutumia muda pamoja Naye? (Sikiliza kwa makini na uthibitishe ushiriki wako.)
4. Nyakati zingine tunafikiri tunahitaji kuwa katika hali fulani au mfumo fulani wa akili kabla ya kukutana na Yesu au kumruhusu aingie katika nyumba yetu au moyo wetu.

Leo tutagundua kile kinachomaanisha kuja kwa Yesu jinsi tulivyo, bila kubadili kitu chochote kwanza.

GUNDUA

Hebu tuombe na kumsihi Roho Mtakatifu atufundishe Neno.

Endelea Kuja kwa Yesu Kama Ulivyo Kila Wakati!

Soma: Mathayo 11:28-30
Uliza: Ni wakati gani tunakuja kwa Yesu? (Jibu kwa kutumia Maandiko ya Biblia tu.)

Omba mrejesho wa kikundi. Ruhusu mjadala. (Anasema wakati tunapokuwa tumechoka na kulemewa na mizigo, ndipo tunapokuja Kwake.)

Soma: Luka 5:30-32
Uliza: Kwa mujibu wa Yesu, ni sifa gani inatupatia hadhi ya kuja Kwake? (Tunapokuwa wagonjwa/ tunapokuwa na wenye dhambi!)

Yesu anakualika kuja Kwake katika madhabahu kila siku ukiwa kama ulivyo. Unapokuwa mgonjwa na unashangaa kwa nini haingilii kati, unapokuwa umechoka na unahisi kutojali kitu chochote au mtu ye yote, unapokuwa umetenda dhambi dhidi ya Mungu au watu na unahisi kuaibika sana kumwendea Mwana wa Mungu asiye na doa—njoo Kwake hata hivyo! Njoo Kwake unapokuwa umekata tamaa na unahisi kuwa mkiwa. Njoo Kwake wakati giza linapokusonga na unahisi kugubikwa na huzuni kubwa. Njoo Kwake ukiwa na hasira kwa sababu hakuja au hakukulinda na wakati maombi yako yanaonekana kutokujibiwa.

Njoo Kwake katika mazingira ya kila yo yote. Hatakufukuza.

Ushuhuda wa Mwandishi

Nilipokuwa kijana mdogo, nilipata ajali mbaya nilipokuwa nikikimbia nikiwa juu ya mgongo wa farasi nikiwa na rafiki yangu. Tulikuwa tukikimbia tukiwa migongo wazi (bila tandiko) katika shamba ambalo limelimwa kwa plau. Wakati farasi wangu aliporuka kwenda mbele kukatiza shamba lililokatwa kwa plau,

Mikono yangu iliachia nikaanguka chini ya kwato zilizokuwa zikiponda ardhi!

Farasi alikanyaga mguu wangu wa kulia viabaya sana. Rafiki yangu alinichukua na kunirudisha nyumbani, ambapo nilijaribu kuuhudumia mguu wangu wakati wazazi wangu walipokuwa nje ya mji. Siku moja baadaye, wazazi wangu walirudi. Mama yangu aliuangalia mguu wangu uliojeruhiwa vibaya na aligundua kuwa mguu wangu ulikuwa umevimba na ulikuwa na rangi ya ajabu.

Alinichukua kwenda kumwona daktari—kama nilivyokuwa. Daktari aliupima mguu wangu na aliniuliza kwa umakini, "Kijana, unataka kubaki na mguu wako?" "Ndiyo, bwana!" Nilisema. "Sasa lazima uende hospitali mara moja ili wafanye kazi ya kuuokoa mguu wako kabla ya kulazimika kuukata. Hakuna damu inayotiririka kwenda kwenye unyao wako!"

Ninamshukuru daktari wangu aliyeniona jinsi nilivyokuwa, lakini nashukuru pia kwa sababu hakuniacha katika hali ile ile. Bado nina mguu wangu na wayo wangu na natembea au kukimbia kwa furaha takribani kila siku! Asante Mungu kwa ajili ya madaktari wanaotupokea kama tulivyo! Asante Mungu kwa ajili ya Yesu anayefanya hivyohivyo!

Yesu alisema, "Wenye afya hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye haki, bali wenye dhambi." (Marko 2:17).

Yesu anakuchukua jinsi ulivyo. Hauhitaji kujaribu kujiponya kabla ya kuja Kwake. Yeye peke Yake ni Mponyaji. Anajitolea kukuponya ndani na nje! Yeye nid Daktari anayekaa na wewe wakati wa mchakato wa uponyaji na milele zote. Anasema, "... Sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa" (Ebr. 13:5). Hii ni ahadi Yake kwako.

Ellen White aliandika:

> Unapoona hali ya dhambi, usisubiri kujifanya kuwa bora zaidi. Ni wangapi wanaofikiri kuwa hawastahili kuja kwa Kristo. Unatarajia kuwa bora zaidi kwa juhudi zako binafsi? "Je! Mkushi aweza kuibadili ngozi yake, au chui madoa-doa yake? Kama aweza, ndipo na ninyi mwaweza kutenda mema, ninyi mliozoea kutenda mabaya." Yeremia 13:23. Kuna msaada kwa ajili yetu

> kwa Mungu peke yake. Hatupaswi kusubiri kwa ajili ya ushawishi mkubwa zaidi, kwa ajili ya fursa kubwa zaidi, au kwa ajili ya hisia takatifu zaidi. Hatuwezi kufanya jambo lolote kwa ajili yetu wenyewe. Inatupasa kuja kwa Kristo kama tulivyo (Steps to Christ, uk. 31).

Unaweza kumtumaini Yesu sasa hivi na milele zote. Anatarajia kuja kukuchukua na kukupeleka mbinguni ukaye Naye. Anasema, "I will come again and receive you to Myself, that where I am, there you may be also" (Yohana 14:3). Lakini unaweza ukawa unashangaa, "Je, naweza kuwa tayari kumlaki Yesu?"

## Gundua Jinsi Unavyoweza Kuwa na Hakika ya Wokovu Wako!

Ikiwa Yesu angerudi jioni ya leo, ungeenda mbinguni? Kwa nini ungekwenda au kwa nini usingekwenda?

Njoo madhabahuni—njoo kwa Yesu kama ulivyo— na ujue kuwa unaweza kuwa na hakika juu ya wokovu wako. Unapokuja kwa Yesu, kumbuka kuwa unakuja pia kwa Mungu Baba ambaye anakupatia wokovu katika Yesu!

Kidokezo cha Kiongozi

- Zifahamu hatua hizi ili uweze kutumia maneno yako mwenyewe badala ya kutumia maandishi. Ingekuwa vizuri kusoma aya ya Biblia na kikundi au vikundi na uliza swali kabla ya kutamka hatua. Kwa njia hii, utawaongoza wanakikundi kulisikia Neno la Mungu kwanza na kufikiri kuhusu maana yake kabla ya kutoa jibu na kutoa hitimisho la hatua.
- Ongeza ahadi za Biblia zenye umhimu kwako kama kiongozi.

Sasa tunakwenda kujifunza hatua saba sahili zinazotuonesha tunavyoweza kuwa na hakika ya wokovu.

## Hatua Saba – Kuwa na Hakika ya Wokovu!

Soma: Warumi 5:8
Uliza: Unajuaje kuwa Mungu anakupenda?

Soma: Warumi 8:38, 39
Uliza: Kuna kitu chochote kinaweza kututenga na upendo wa Mungu?

Hatua #1 – Unaweza kuwa na hakika kuwa hakuna kitu chochote kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu.

Soma: Warumi 3:23
Uliza: Ni tatizo gani ambalo sisi sote tunalo?

Soma: Warumi 6:23 (sehemu ya kwanza)
Uliza: Matokeo ya dhambi yetu ni nini?

Hatua #2 – Unaweza kuwa na hakika kuwa, kama mwenye dhambi, unamhitaji Mwokozi.

Somo: Warumi 6:23 (sehemu ya kwanza) na Waefeso 2:8, 9
Uliza: Ni zawadi gani unayopewa bure na Mungu?

Hatua #3 – Unaweza kuwa na hakika kuwa wokovu ni zawadi ya Mungu ya bure kwako.

Soma: Yohana 3:16
Uliza: Ni kwa jinsi gani zawadi hii ya uzima wa milele inakuwa ya kwako?

Hatua #4 – Unaweza kuwa na hakika kuwa Yesu ni Mwokozi wako unapomwamini.

Soma: Ufunuo 3:20
Uliza: Jibu lako kwa jibu kwa ombi la Yesu?

Hatua #5 – Unaweza kuwa na hakika kuwa Yesu anataka kufanya makazi katika moyo wake kwa imani.

Soma: 1 Yohana 1:9
Shiriki: Tunapoungama dhambi zetu na kumwalika Yesu awe Mwokozi wetu binafsi, anakuja katika moyo wetu mara moja kwa imani kwa njia ya Roho Mtakatifu. Anakuja katika haki Yake, usafi na ukamilifu wake. Tunagundua zaidi kuliko hapo awali ni kiasi gani tunamhitaji Yesu asafishe mioyo yetu.
Uliza: Yesu anakufanyia nini unapoungama dhambi?

Hatua #6 – Unaweza kuwa na hakika kuwa Yesu anausafisha moyo wako kabisa.

Soma: 1 Yohana 5:13
Uliza: Aya hii inakuambia jambo gani ambalo unaweza kulielewa kwa hakika?

Hatua #7 – Unaweza kuwa na hakika kuwa Yesu anakupa uzima wa milele.

Mungu anatuambia katika Ufunuo 7:9 kuwa kutakuwa na umati mkubwa wa watu wasiokuwa na idadi wa watu waliookolewa. Mungu amepanga uwe mmoja wao!

Kuja kwa Yesu kama tulivyo kunatufanya kuishi katika amani Yake. Yesu alisema, "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga." (Yohana 14:27).

Kuja kwa Yesu kama Mwokozi wetu hutuwezesha kuishi katika furaha Yake! "Naye mwampenda, ijapokuwa hamkumwona; ambaye ijapokuwa hamwoni sasa, mnamwamini; na kufurahi sana, kwa furaha isiyoneneka, yenye utukufu, katika kuupokea mwisho wa imani yenu, yaani, wokovu wa roho zenu." (1 Petro 1:8, 9).

Baba Mungu wetu ni Mpaji wa zawadi zote njema kwako (Yakobo 1:17). Zawadi hizi zisizokuwa na kikomo hujumuisha wokovu, uzima wa milele, moyo mpya, amani, na furaha.

JIZOEZE

1. Soma Ufunuo 3:20 tena ukiwa peke yako na mwalike Yesu ndani ya moyo kama Mwokozi wako.
2. Je, uko tayari kuja kama ulivyo na kuweka maisha yako amana kwa Yesu kama Mwokozi wako?
3. Omba kama ifuatavyo:

> "Baba mpendwa uliye Mbinguni, Wewe ni Mpaji wa zawadi ya wokovu. Sisi ni wenye dhambi tunaomhitaji Yesu kama Mwokozi wetu. Tunakushukuru kwa kumtuma Yesu afe ili tuweze kuwa na uzima wa milele na kufunikwa kwa haki Yake kamilifu. Tunachagua kuamini kuwa zawadi hii ya wokovu na haki ni yetu sasa. Tunamwomba Mwanao, Yesu, aje katika mioyo yetu kwa imani awe Rafiki yetu, Mwokozi na Bwana wetu. Tunaziungama dhambi zetu na tunadai msamaha Wake na utakaso wa udhalimu wetu wote. Asante kwa kuwa tunaweza kuwa na hakika ya uzima wetu wa milele tukiwa na Yesu Mwokozi wetu. Katika jina la Yesu, Amina."

Dondoo hii kutoka Steps to Christ inatia moyo:

> Wakati ahadi kubwa za Biblia zikiwa mbele yako, unaweza kutoa nafasi kwa ajili ya mashaka? Unaweza kuamini kuwa wakati mwenye dhambi maskini anapotamani kurudi, anapokuwa na shauku ya kuacha dhambi zake, Bwana amzuie kwa ukali asije kwenye nyayo Zake kwa ajili ya kufanya toba?
> Mawazo kama hayo yapotelee mbali kabisa! Hakuna jambo linaweza kujeruhi roho yako zaidi kuliko kuwa na dhana kama hiyo moyoni kumhusu Baba yetu wa mbinguni. Anachukia dhambi, lakini anampenda mwenye dhambi, na alijitoa Mwenyewe katika nafsi ya Kristo, ili wote wanaopenda waweze kuokolewa na kuwa na baraka katika ufalme wa utukufu. Lugha gani yenye nguvu zaidi au iliyo laini zaidi angeweza kuitumia kuliko ile aliyoichagua kuelezea upendo

> Wake kwetu? Anatangaza, “Mwanamke anaweza kumsahau mtoto wake mchanga anayenyonya, wala asiwe na huruma kwa mwana mwana wa tumbo lake mwenyewe? Ndiyo, hao wanaweza kusahau, lakini Mimi sitawasahau kamwe.” Isaya 49:15 (Steps to Christ, uk. 54).

## CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 1

Kila wakati, jizoeze kuja kwa Yesu kama ulivyo: mwenye furaha, mwenye huzuni, ukiwa umeshindwa, au ukiwa umeshinda. Kuwa na hakika ya wokovu wetu katika Yesu kunatupatia uhuru kurudi Kwake kila wakati.

Rudi nyumbani na pitia upya hatua saba za uhakika wa wokovu na shiriki hatua hizo na mtu mwingine.

## Kila Siku...
# Mheshimu Yesu kama Bwana

Ni rahisi kumkiri Yesu kama Mwokozi wetu! Hata hivyo, alitubeba kama tulivyo—waliovunjwa na waliopondwa na waliosambaratishwa na dhambi—na ndipo alitukomboa, alitusafisha kwa damu Yake, na alituweka huru kabisa. Kwa sababu hiyo, tunaimba kwa furaha, "Yesu ni Mwokozi wa ajabu kiasi gani, ni Mwokozi wa ajabu kiasi gani!" Lakini, ni jambo tofauti kabisa kumkiri Yesu kama Bwana na wakati huo huo kuimba kibwagizo kinachosema, "Yote kwa Yesu."Hii ni kwa sababu ikiwa Yesu ni Bwana kweli kweli, maisha yetu na mtindo wetu wa maisha utabadiika, na nyakati zingine hatutaki jambo  hilo kwa sababu tunajisikia kupoteza utawala juu ya maisha yetu.

Tafakari juu ya dondoo ifuatayo:

> Siyo ushahidi wa kutosha kuwa mtu ni Mkristo kwa sababu anaonesha msisimko wa kiroho katika mazingira yasiyokuwa ya kawaida. Utakatifu siyo tukio la msisimko: ni kujisalimisha kabisa kwa mapenzi ya Mungu; ni kuishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu; ni kutenda mapenzi ya Baba yetu wa mbinguni; ni kumtumaini Mungu katika majaribu, katika giza hali kadhalika katika nuru; ni kutembea kwa imani na siyo kwa kuona; ni kumtegemea Mungu kwa uhakika usiyo na maswali, na kupumzika katika upendo Wake (The Acts of the Apostles, 51.2).

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapojiandaa kufundisha) kanuni hii ya Kurudi Madhababuni, mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu akufundishe Neno la Mungu katika njia mpya na inayoelewaka kwako mpaka uimbe kwa upendo "Yote kwa Yesu" kwa sababu upendo wa Mwokozi wako umeuteka moyo wako kweli kweli.

Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo

JALI

1. Mwulize kila mwana kikundi: Ni jambo gani jema sana lilitokea kwako leo? (Tumia muda wa kutosha kusikiliza; sherehekea mambo mema na uwe na huruma kwa wale walio na siku ngumu.)
2. Pitia upya kanuni ya Kurudi Madhabahuni uliyojifunza hadi wakati huu:
   - Kanuni 1 – Njoo kwa Yesu kama ulivyo! Kila wakati, jizoeze kuja kwa Yesu kama ulivyo: mwenye furaha, mwenye huzuni, mwenye wasiwasi, mwenye amani, mwenye kushindwa, au mwenye kushinda. Na kumbuka kuwa unaweza kuwa na hakika ya wokovu wako.
3. Uliza: Je, mtu yeyote alishiriki hatua saba sa wokovu na mtu mwingine yeyote?
4. Fundisha: Shirikiana na mtu mwingine na uliza, "Ni kwa namna gani Mungu alikusaidia kukabiliana na changamoto tangu juma lililopita?" Wape jozi dakika 2-3 za kujadiliana. Halafu uliza kundi lote ikiwa mtu yeyote angependa kusema kile ambacho Mungu alikifanya katika maisha yake alipokubali changamoto ya kuja kwa Yesu kama alivyo.

UNGANISHA

1. Kutateni katika timu za watu wawili wawili. Uliza: "Ni mtu gani unamheshimu zaidi kuliko watu wengine wote na kwanini?" Baada ya dakika 2–3 za majadiliano, uliza ikiwa mtu ye yote anaweza kueleza kundi zima.
2. Swali: Ni sifa zipi za mtu tunaziheshimu zaidi kuliko sifa zingine zote? (Ruhusu mjadala wa wazi.) Ni kwa jinsi gani sifa hizi zinahusiana na uhusiano wetu na Yesu? (Sikiliza kwa makini na thamini uhusikaji.)

Leo tutachunguza nini maana ya kumheshimu Yesu kama Bwana.

GUNDUA

Omba: "Baba wa mbinguni, tafadhali mtume Roho Mtakatifu atufundishe Neno Lako. Katika jina la Yesu, amina."

Aya zifuatazo zinatuambia nini kuhusu Yesu?

Soma: Marko 1:35
Asubuhi na mapema, Yesu aliamka wakati bado ni giza na kwenda nje mahali pa upweke ili kuomba.

Soma: Isaya 50:4
Uliza: Ni nani anashuhudia katika aya hii: Isaya mtoa unabii au mtu mwingine?

Soma: Isaya 50:6 kugundua jibu.

Huu ni unabii unaomhusu Masihi ukielekeza kwa kile ambacho Yesu angekipitia kila asubuhi akiwa katika dunia hii.

Kila asubuhi, Mungu angemwamsha Yesu ili amfanye Mwanafunzi/amfundishe. Mungu angempa ulimi wa mwanafunzi/mwalimu ili ampe neno la kumtegemeza aliyechoka. Muda huu wa asubuhi na mapema ulikuwa kiini cha maisha ya Kristo duniani.

Baba wungu yetu anatupenda sana kiasi ambacho anatuamsha kama alivyomwamsha Masihi! Atatuleta madhabahuni kila asubuhi.

Ni upendo wa Baba unaosukuma moyo Wake kutuamsha kila asubuhi ili tuwe na wakati usiokuwa na haraka pamoja Naye, Mwanae, na Roho Mtakatifu.

## Sehemu I – Mheshimu Yesu Kama Bwana

Mheshimu Yesu kama Bwana kwa kumwomba Mungu kila usiku akuamshe asubuhi inayofuata ili uwe na muda usio na haraka, usioingiliwa ukiwa peke yako Naye katika Neno na maombi.

Swali: Neno la Mungu linatufundisha nini kuhusu kuhusu Yesu kama Bwana?

Soma: Mathayo 28:18
Yesu alitangaza kuwa amepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.

Soma: Wafilipi 2:5–11
Yesu alijinyenyekesha ili amtii Mungu Baba hadi akafa msalabani. Yesu alikuwa na walifufuka kutoka kaburini. Mungu alimwinua Yesu na kumketisha mkono Wake wa kulia na alimpa jina lipitalo majina yote. Kwa jina la Yesu, kila goti litapigwa na kila ulimi utamkiri Yeye kama Bwana.

Tunajua kuwa kila mmoja katika yunivesi siyo muda mrefu atapiga magoti kwa Ubwana wa Yesu Kristo. Kwa hiyo, kwa nini tusimheshimu Yesu kama Bwana sasa? Tunampenda Yesu kama Rafiki na Mwokozi lakini siyo kama Bwana wetu?

Shughuli/Mfano wa Kiti cha Dereva

- Panga viti vinne badala ya viti vinne vya gari ndogo ya kufikirika (kiti cha dereva, kiti cha msafiri, viti vya nyuma viwili).
- Furahia kueleza gari la kifahari jipya kabisa na uliza mtu angependa kujitolea kuwa dereva wa gari hili jipya.
- Wakati mtu anayejitolea anapokuja mbele, anza mjadala ufuatao.

Jenga muktadha wa simulizi: Wewe umekalia kiti cha dereva wa maisha yako. Unaamua unapotaka kwenda, jinsi unavyotaka kufika pale, na ni kwa haraka kiasi gani ufike pale. Lakini ndipo unaamua kuwa unataka Yesu awe Bwana wa maisha yako. Ikiwa Yesu ni Bwana wa maisha yako, anapaswa kukaa wapi katika gari hili? (Kipatie kikundi muda wa kujibu; watamweka Yesu katika kiti cha dereva. Fuata muhtasari wa simulizi.)

Uliza 1: Ikiwa Yesu sasa yupo katika kiti cha dereva, utakuwa umekaa wapi? (Kipatie kikundi muda wa kujibu. Kwa kawaida

watajiweka katika kiti cha msafiri kando ya Yesu. Cheza na jinsi wanavyojibu.)

Uliza 2: Kwa hiyo, Yesu anaendesha gari sasa. Kunatokea nini wakati Yesu anapoelekea katika upande usiotaka kwenda? (Ruhusu muda kwa ajili ya jibu na halafu onesha kwa kunyakua usukani kutoka kwa Yesu.)

Uliza 3: Nini kitatokea ikiwa Yesu haendeshi kwa kasi unayoitaka? (Kipatie kikundi muda wa kujibu na halafu onesha jinsi unavyoweza kusukuma mguu kutokea upande wa kiti cha msafiri hadi kanyagio la petroli ili kuongeza kasi ya mwendo wa gari.)

Uliza 4: Hebu uliza tena: Ikiwa Yesu ni Bwana wa maisha yako, unapaswa kukaa wapi? (Toa muda kwa kikundi kujibu. Ikiwa wanapendekeza kiti cha nyuma, kubaliana nao. Ikiwa watapendekeza buti, ruka na kwenda kwa wazo la mwisho.)

Uliza 5: Ikiwa umekaa katika kiti cha nyuma na Yesu anaanza kuelekea katika upande tofauti na ule unaoutaka, unafanya nini? (Toa muda kwa ajili ya jibu. Unajua kile ambacho nyakati zingine nakifanya? Ninaanza kulalamika na ninajaribu kumwambia kutokea kiti cha nyuma kuwa anaelekea upande usiokuwa sahihi.)

Uliza 6: Ikiwa Yesu ni Bwana wa maisha yako, unapaswa kukaa wapi? (Toa muda kwa ajili ya jibu. Hadi sasa washiriki wanapaswa kujiweka katika buti la gari.)

Wazo la Mwisho: Sawa! Unajua mahali pazuri zaidi kwa ajili yetu kuwa kama Wakristo wakati Yesu anapokaa katika kiti cha dreva, wakati Yeye ni Bwana wa maisha yetu? Tunapaswa kuwa ndani ya buti. Hatuwezi kuona mahali tunapokwenda, na hatuwezi kumwambia Yesu cha kufanya. Lakini tunalala chini katika imani sahili, tukitumaini kuwa Bwana na Mwalimu wetu atatupeleka mahali anapojua tunapaswa kuwa.

Omba: Funga mfano kwa ombi, ukiomba kuwa tujisalimishe kwa Yesu kama dereva na BWANA wa kila eneo la maisha yetu.

## Kurudi katika Neno!

Swali: Tunawezaje kuacha kufanya mambo tunayojua kuwa siyo sahihi?

Soma: Ezekieli 36:26, 27
Yesu yuko tayari kukata na kuondoa maeneo magumu katika mioyo yetu yanayokataa Ubwana Wake. Inatupasa kujisalimisha kwa Yesu kama Dakatari Bingwa wa Upasuaji ili aweze kufanya upasuaji huu kwa ajili yetu.

Somo: Wakolosai 1:27, 28
Siri ya ushindi ya Mkristo imo katika virai viwili vya maneno matatu katika aya hii. Ni maneno gani hayo? ("Kristo ndani yako" na "kamili katika Kristo")

Yesu anaishi ndani yetu, kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu, na anawezesha kujisalimisha kwetu! Wakati haki yetu ni kama nguo iliyotiwa unajisi (tazama Isa. 64:6), sisi ni wakamilifu katika Kristo.

Yesu aliishi maisha kamili ya kujisalimisha kwa Baba Yake wa mbinguni kila wakati na kila siku. Yesu alisema, "Chakula changu ndicho hiki, niyatende mapenzi yake aliyenipeleka" (Yohana 4:34). Shauku ya Yesu ilikuwa kufanya mapenzi ya Mungu Baba.

Katika Bustani ya Gethsemane, Yesu alilemewa na uzito wa kila dhambi iliyotendwa na kila mtoto, kila kijana, na kila mtu mzima aliyewahi kuishi. Alitafuta njia ya kuepuka mateso hayo kutoka kwa Baba Yake—lakini angalia alivyoomba alipoangukia uso Wake: "...Baba yangu, ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke; walakini si kama nitakavyo mimi, bali kama utakavyo wewe" (Mathayo 26:39, mkazo umeongezwa). Mara tatu alipigana mieleka na kile alichokitaka Yeye binafsi na alichagua kuachana na mapenzi Yake ili kufuata mapenzi ya Baba Yake.

Yesu yule yule, ambaye kila siku aliacha mapenzi Yake kwa Baba Yake, anaishi ndani yako kwa njia ya Roho Wake Mtakatifu. Yesu yule yule, ambaye alitaka kuishi na asife, alitoa mapenzi Yake kwa Baba Yake, alinyosha mikono Yake, na kujisalimisha afe msalabani mahali pako! Ukweli huu mtukufu unatuongoza kuwa tayari kusalimisha vyote Kwake kila siku!

Tunaweza kufanya nini kila asubuhi kuondoa kila kishawishi kila asubuhi ili tuuheshimu Ubwana wa Yesu?

“Tazama, Mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu!” (Yohana 1:29).

## Sehemu II – Mheshimu Yesu kama Bwana

Kila asubuhi, hebu iwe kipaumbele chako cha kwanza kuelekeza moyo wako kwa kile alivyo Yesu na kile ambacho amekutendea. Halafu salimisha vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, na hata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.

Yesu huyu huyu, ambaye ana nguvu zote na mamlaka yote ndani yako; anakupa nguvu na mamlaka ya kusalimisha mapenzi yako Kwake. Yesu atakusaidia! Hatakuangusha kamwe!

Neno la Mungu linafundisha nini kuhusu Chanzo cha nguvu kwa ajili ya Kristo?

Soma: Waefeso 2:22 na Wafilipi 2:13
Baba na Mwana huishi nasi (huishi ndani yetu) kupitia kwa Roho Mtakatifu. Na ni neema ya Mungu Mwenyewe inayotupatia nguvu ya kujisalimisha. Anatupatia uwezo wa kutaka na uwezo wa kutenda mapenzi Yake.

Soma: Yohana 14:17-18, 23 na Waefeso 3:14–19
Hatuko peke yetu katika kupambana, kuwa na wasiwasi, na kujitahidi kujaribu kumheshimu Yesu kwa siku nzima. Sisi siyo

yatima wa kiroho! Yesu aliahidi, “Sitawaacha yatima; nitakuja kwenu.” Na wakati atakapokuja kwetu, tutauona ukamilifu Wake.

Mfano wa Bahari/Kikombe

- Vifaa vinavyohitajika: sufuria ya maji, kidondosha macho, kikombe
- Weka sufuria ya maji mezani.
- Eleza kuwa sufuria ya maji ni bahari, na bahari inamwakilisha Yesu na ukamilifu Wake.
- Eleza kuwa kikombe kinakuwakilisha wewe.
- Kwa kukutumia kidondosha macho, weka matone machache ya maji katika kikombe.
- Uliza, “Bhari iko ndani ya kikombe?” Tone dogo tu!
- Unataka Yesu akae ndani yako katika ukamilifu wote kwa njia ya Roho Wake, hivyo unafanyaje? Unazama ndani ya bahari.
- Zamisha kikombe cha maji katika sufuria ya maji. Hii ndiyo maana ya kukaa ndani ya Yesu. Kwa kadiri unavyozama ndani ya Yesu, ndivyo Naye atakuwa ndani yako, na ndivyo utakavyofanana Naye zaidi.
- Kwa kusudi la mkazo wa injili, uliza tena: “Je, bahari iko ndani ya kikombe au kikombe kiko ndani ya bahari?”
- Jibu sahihi: Wakati sehemu ndogo ya bahari iko ndani ya kikombe, kikombe bado kiko ndani ya bahari!

Kama vile Yesu anavyoishi ndani yetu kwa imani (kikombe kilichojaa maji) na anatuwezesha kujizaa matunda mema, tunadumu pia kukaa ndani Yake, na maisha Yake hutiririka katika maisha yetu.

> Mungu anatamani kuonesha kupitia kwako utakatifu, ukarimu, huruma, na tabia yake Mwenyewe. Lakini Mwokozi hawaagizi wanafunzi kufanya kazi ili wazae matunda. Anawaambia wakae ndani Yake. “Mkikaa ndani Yangu,” Anasema, “na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni neno mtakalo lo lote, nanyi mtafanyiwa.” Ni kwa njia ya neno ambapo Kristo nakaa

> ndani ya wafuasi Wake. Huu ndiyo muungano muhimu unaowakilishwa na kuula mwili Wake na kuinywa damu Yake. Maneno ya Kristo ni roho na uzima. Ukiyapokea, unapokea uzima wa Mzabibu. Unaishi "kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Mathayo 4:4. Uzima wa Kristo ndani yako huzalisha matunda yale yale yaliyomo ndani Yake. Kuishi ndani ya Kristo, kushikamana na Kristo, kuungwa mkono na Kristo, kupata chakula kutoka kwa Kristo, unazaa matunda yanayofanana na Kristo (The Desire of Ages, uk. 677, mkazo umeongezwa).

Kazi yetu kubwa kuliko zote siyo kuzaa matunda bali kukaa ndani Yake!

Soma: Wafilipi 4:13 "Nayaweza mambo yote katika Yeye (Kristo) anitiaye nguvu."

Kristo ndiye nguvu yetu ya kuishi kila wakati kwa kumheshimu Yeye. Tunapokuwa ndani Yake, na Yeye akiwa ndani yetu, tutaka kuishi kwa ajili ya heshima na utukufu Wake. (Tazama 1 Kor.10:31.)

Soma: Wafilipi 4:8
"Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo."

## Sehemu III – Mheshimu Yesu Kama Bwana

Kila wakati, jizoeze kumheshimu Yesu kwa chaguzi zako. Ndiyo, unaweza kuanza leo!

JIZOEZE

Mara nyingi tunamjua Yesu kama Mwokozi na Rafiki, lakini tunamjua kama Bwana?

1. Chora mstari katikati ya kipande cha karatasi.
2. Katika upande mmoja wa mstari, chora taji juu. Chini ya taji, andika "Kile ambacho kimesalimishwa kwa Yesu." Katika safu hiyo, orodhesha mambo ambao unayajua umeyakabidhi kwa Ubwana wa Yesu (yale ambayo umeyasalimisha Kwake).
3. Katika upande mwingine, andika "Kile ambacho hakijasalimishwa kwa Yesu." Katika safu hiyo, andika mambo ambayo unapambana nayo kuyasalimisha. Baada ya kuandika mambo machache, omba na mwulize Roho Mtakatifu ikiwa kuna jambo lo lote umelisahau.



| **Kili**chosalimishwa kwa Yesu | **Kisi**chosalimishwa kwa Yesu |
|---|---|

Chochote kile ambacho hakijasalimishwa kwa Ubwana wa Yesu hutushikilia kama watumwa.

Weka chati hii kando ya kitanda chako na, kila siku wiki hii ijayo, salimisha kile ambacho hakijasalimishwa kwa Yesu. Ikiwa unapambana kukisalimisha, omba, "Bwana nifanye mimi nitake kujisalimisha!" Unaweza kuongeza "mambo mengi unayoyapenda" kwa kadiri unavyohitaji katika ombi hilo.

Wito wa Kiongozi

Ni nani anayemhitaji Yesu kufanya kile alichokiahidi katika Ezekieli 36:26, 27: kukupatia moyo mpya na kuondoa moyo wako wa jiwe?

Ikiwa Mungu anakuita upate upasuaji huu wa moyo, tafadhali ungana nami kwenye magoti yako mbele za Bwana.

Ninakualika uwe na ombi binafsi ukimwomba Yesu aondoe chochote katika moyo wako ambacho hakitakiwa kuwepo hapo: uchungu, chuki, tamaa mbaya, au upendo kwa ajili ya kitu chochote au mtu yeyote anayechukua nafasi ya Bwana.

Omba: "Baba mpendwa uliye mbinguni, asante kwa kutupenda sana! Asante kwa ajili ya Yesu, Mpasuaji wetu Mkuu. Tunaomba kuwa Yesu aje, kwa nguvu ya, kwa njia ya Roho Mtakatifu, na uondoe sehemu ngumu katika mioyo yetu. Tafadhali ondoa uchungu wetu, maumivu yetu, na upendo wetu kwa ajili ya kitu chochote kinachochukua nafasi ya Yesu kama Bwana. Tupatie mioyo mipya! Amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 2
Juma hili linalokuja, unapotafuta kumheshimu Yesu kama Bwana,  jitahidi kufanya yafutayo:

Sehemu I: Mwombe Mungu akuamshe kila asubuhi uwe na muda usiokuwa na haraka ukiwa peke yako pamoja Naye.
Sehemu II: Kila asubuhi, fanya kuwa kipaumbele chako cha kwanza kuelekeza mawazo yako yote kwa Yesu kama Bwana na kwa kile ambacho Yesu amekifanya kwa ajili yako. Halafu salimisha vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, n ahata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.
Sehemu III: Kwa nguvu ya Yesu anayeishi ndani yako kwa imani, fuata uongozi katika chaguzi zako zote katika siku nzima.

Daima kumbuka…

Yesu anasema, "pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lo lote." Ukuaji wetu katika neema, furaha yetu, kufaa kwetu kwa utumishi —vyote hutegemea muungano wetu na Kristo. Ni kwa njia ya mawasiliano Naye, kila siku, kila saa,—kwa kukaa ndani Yake—ambapo tunakua katika neema. Siyo tu kuwa Yeye ni Mwasisi, bali pia ni Mkamilishaji wa imani yetu. Ni Kristo mwanzo na mwisho na wakati wote. Yeye anapaswa kuwa nasi, siyo tu mwanzoni naka mwishoni mwa safari yetu, bali katika kila hatua ya njiani. Daudi anasema, "Nimemweka Bwana mbele yangu daima, Kwa kuwa yuko kuumeni kwangu, sitaondoshwa." Zaburi 16:8 (Steps to Christ, uk. 69).

## Kila Siku...
# Mgundue Yesu katika Neno Lake na katika Maombi

Neno la Mungu lililoandikwa ni barua Yake binafsi ya upendo kwa mioyo yetu. Ndani yake tunagundua Mungu ni nani, sisi ni nani, na kile anachotamani kukifanya ndani yetu na kupitia kwetu kama watoto Wake. Neno Lake ni takatifu, linaaminika, na linaendana na wakati. Neno Lake ni mamlaka ya juu na ni nuru isiyozimika inayoang'aa gizani.

Wakati Neno la Mungu lililoandikwa ni nanga ya imani yetu na ya uhusiano wetu Naye, maombi ni pumzi ya roho yetu! Maombi bila Neno huongozwa na mhemko na sawa na meli isiyokuwa na usukani. Neno bila maombi binafsi halina uhai na limevunda, sawa na mkate wa zamani uliosahauliwa nyuma ya kabati.

Maombi ni jinsi tunavyozungumza na Mungu, na, kujibu, anaongea na akili zetu kupitia Roho Mtakatifu na tunaposoma na kutafakari Neno lililoandikwa. Kama vile mahusiano ya kibinadamu yasivyoshamiri bila mawasiliano, kadhalika uhusiano wetu na Mungu hauwezi kudumu, acha tu kushamiri, bila mawasiliano ya kila siku Naye.

Mungu anapenda tunapoongea Naye katika maombi. Hakuna maneno ya kufikirika yanayohitajika. Anataka tu kuusikia moyo wetu.

> Maombi ni kufungua moyo kwa Mungu kama kwa rafiki. Siyo kwa sababu ni lazima ili tujitambulishe kwa Mungu kuwa sisi ni nani, bali ili tuweze kumpokea Yeye. Maombi hayamleti Mungu chini kwetu, bali yanatupandishwa Kwake. Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani aliwafundishwa wanafunzi Wake jinsi ya kusali. Aliwaelekeza kuwasalisha mahitaji yao ya kila siku

> mbele za Mungu, na kutupa mashaka yao yote Kwake. Na uhakika aliowapa kuwa maombi yao yatajibiwa, ni uhakika kwetu pia (Steps to Christ, uk. 93).

Mungu anafurahia kuzungumza nasi, na anatamani tuviinue vichwa vyetu na kufurahi ndani yake kila siku!

"Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu, Asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia" (Zaburi 5:3).

"Mausia yako ni matamu sana kwangu, Kupita asali kinywani mwangu!" (Zaburi 119:103).

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapojiandaa kufundisha) somo hili la Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu azungumze na moyo wako katika namna ambayo ina mguso mkubwa kiasi kwamba uwe unapata njaa kwa ajili ya muda mwingi zaidi katika Neno la Mungu na maombi.

Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo

JALI

1. Waombe wanakikundi waulizane wao kwa wao: "Ni wapi ulimwona Mungu akifanya kazi katika maisha yako juma hili lililopita?"
2. Uliza: Ni kanuni zipi za Kurudi Madhabahuni umejifunza mpaka sasa?
    - Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo!
    - Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana.
        - Sehemu I: Mwombe Mungu akuamshe kila asubuhi ili uwe na muda usio na haraka wa kuwa pamoja wewe peke yako na Yeye.
        - Sehemu II: Kila asubuhi, fanya iwe kipaumbele chako kutafakari juu ya Yesu ni nani na amefanya nini kwa ajili yako. Halafu jisalimishe vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, hata mtazamo wa na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.

- Sehemu III: Kwa nguvu ya Yesu anayeishi ndani yako kwa imani, fuata uongozi Wake katika chaguzi zako katika siku nzima.

3. Kaeni katika vikundi vya watu wawiliwawili. Uliza: "Mungu alikusaidiaje kuishi changmoto ya juma lililopita?" Changamoto ilikuwa kumruhusu Mungu akuamshe, uwe na wakati usio na haraka Naye, umtazame, na ujisalimishe Kwake kama Bwana. Wape watu walio katika vikundi vya watu wawili wawili dakika 2–3 za kujadili. Uliza wanakikundi wote ikiwa kuna mtu ye yote anayependa kueleza kile ambacho Mungu amewatendea katika maisha yao walipoipokea changamoto.

UNGANISHA

1. Wapange wote katika duara. Waite washiriki wafikirie kitu fulani walichokifanya ambacho kilihitaji umakini mkubwa. Mwalike kila mmoja kuigiza shughuli ile iliyohitaji akili zote wakati kikundi kikibuni ni shughuli gani.
2. Ni mambo gani maishani huhitaji umakini mkubwa? Ni umakini wa aina gani tunapaswa kuwa nao tunaposoma Neno la Mungu?

Leo tutachunguza jinsi ya kusoma Neno la Mungu kwa umakini mkubwa.

GUNDUA

Tunapojiandaa kufungua Neno la Mungu, fikiria dondoo ifuatayo:

> Biblia ni sauti ya Mungu inayoongea na sisi, kama vile ambavyo tungeisikia kwa masikio yetu. Ikiwa tunalitambua hili, ni kwa kicho kikubwa kiasi gani tunapaswa kufungua Neno la Mungu, na ni kwa bidii kubwa kiasi gani tunapaswa kutafuta kanuni zake! Usomaji na tafakari ya Maandiko vinapaswa kuchukuliwa kama kuwa na kikao na Yeye Asiye na Kikomo (Testimonies to the Church, vol. 6, uk. 393).

Omba: "Baba wa mbinguni, tunaomba kuwa Umtume Roho Mtakatifu atufundishe umakini tunaopaswa kuwa nao katika Neno Lako na maombi. Tunaomba pia utupatie kicho

na upendo Kwako na kwa Neno Lako. Katika jina la Yesu, amina."

Kwa jinsi gani tunaweza kuwa na muda wa kutosha pamoja na Mungu katika Neno Lake?

Unapofungua Biblia kila siku, unamwomba mwalimu wako akusaidie kuielewa kwa uwazi zaidi?

Soma: 1 Wakorintho 2:12–14 na Yohana 16:13
Uliza: Ni nani anaweza kutusaidia kuuelewa ukweli? (Mwombe Mungu Roho Mtakatifu akuongoze katika ukweli wote!)

Yesu ni ukweli (Yohana 14:6) katika Neno Lake lililoandikwa.

Yesu siyo Bwana wa maisha yetu mpaka pia awe Bwana wa muda wetu. Muda pamoja na Yesu unapaswa kuja kabla hatujasumbuliwa na simu zetu au vifaa vytetu vya kielektroniki, kabla ya kuangalia barua pepe zetu na akaunti zetu za mitandao ya kijamii, na kabla ya kujiingiza katika kazi au biashara zetu. Tunaweza kutambua uongozi wa Roho Mtakatifu vizuri zaidi tunapojifunza Neno wakati sauti Yake haishindani na teknolojia ambayo tayari tumeshaifungua kabla ya Neno! Lengo letu linapaswa kuwa kukutana na Yesu kabla ya kuanza siku yetu au kabla ya kukutana na watu wengine.

(Je, unapambana daima na usumbufu wa vifaa hivyo vya kidijitali au simu janja? Tazama vidokezo katika Kiambatanisho 5  kwa ajili ya tabia zenye afya njema zaidi za kidijitali.)

Soma: Yohana 5:39

Yesu alisema nini kuhusu kiini cha Neno lote la Mungu? (Maandiko yote yanamhusu na yanamshuhudia Yesu.)

Jizoeze: Mpe kila mmoja dakika 5–7 katika makundi ya watu wawili wawili.

1. Linganisha Mithali 12:3 na Zaburi Psalm 16:8. (Nani ni mzizi wa haki?)

2. Linganisha Mithali 12:12 na Yohana 15:1–5.

(Ni kwa jinsi gani unaona picha mpya katika aya hizi?)

Soma: Yeremia 29:13
Inatupasa kumtafuta nani tunapojifunza Neno la Mungu?
(Yesu! Tukimtafuta kwa mioyo yetu yote, tutamwona!)

Shughuli ya Kutafuta Hazina

- Kabla ya kukutana, ficha sarafu chache (au chenji ndogo) katika chumba ambcho vikundi vyako vidogo vidogo hukutana. Zifiche vizuri kabisa!
- Uliza mtu anayejitolea na anayependa kutafuta hazina.
- Mwulize mtu anayejitolea atafute sarafu.
- Ikiwa mtu huyo hazipati, mwulize ni kwa muda gani anapenda kutafuta mpaka azipate? Ikiwa pesa zimepatikana, unaweza bado kuendelea kuuliza kana kwamba hazijpatikana. (Walio wengi watasema wasingekuwa tayari kutafuta kwa muda mrefu kwa sababu hazina thamani kubwa!)
- Sasa, shika noti ya dola $10 (au pesa nyingi zaidi katika fedha za nchi mahalia) na uliza ni kwa muda mrefu kiasi gani wangeendelea kutafuta mpaka waipate. (Ikiwezekana, unaweza kuificha hiyo na kumpa kabisa yule ambaye angeitafuta na kuipata!)
- Sasa onesha noti bandia ya dola $10,000 (au kiasi kikubwa zaidi chapesa) na uliza ni kwa muda mrefu kiasi gani wangeitafuta hadi waipate?
- Wote tungeendelea kuitafuta mpaka tuipate!

"Kama vile mchimbaji wa madini anavyogundua njia za madini yenye thamani yaliyojificha chini ya uso wa ardhi, ndivyo atakavyofanya mtu anayechunguza bila kuchoka Neno la Mungu kwa ajili ya hazina ililositirika anavyopata kweli za thamani kubwa, zilizofichika dhidi ya mtafutaji asiyekuwa makini" (Steps  to Christ, uk. 90).

Omba: Je, ungependa kuomba na kumwuliza Mungu akusaidie kuchunguza Neno Lake kama mtu atafutaye hazina yenye thamani kubwa iliyositirika? Hebu tuombe!

Soma: Mathayo 7:24 na Yohana 14:23
Kipaumbe chetu kinapaswa kuwa kipi baada ya kumpata Yesu katika Neno la Mungu? (Neno la Mungu linapaswa kutekelezwa, siyo kusikiwa tu. Tunavyomheshimu Mungu wa Neno ni mwangwi wa upendo wetu kwa Mungu wa Neno. Tafakari jambo hilo kwa muda!)

Mungu Baba anapenda kutupatia Roho Mtakatifu, ili tuweze kumwona Yesu Kristo katika sehemu ya Neno lililoandikwa! Na tunapomtafuta Yesu, upendo wetu kwa ajili ya Neno Lake utakua.

Tunawezaje kuwa na Muda wa Kutosha na Mungu katika Maombi?

Soma: Zaburi 100:4
Tunapaswa kuanzaje muda wetu katika maombi? (Njoo katika uwepo wa Mungu ukiwa na shukurani na sifa.)

Tofauti kati ya shukurani na sifa ni nini?

- Shukurani inaelekezwa kwa kile ambacho Mungu ametufanyia wewe na mimi: Vitu anavyotupatia, ulinzi, n.k.
- Sifa hutangaza Mungu ni nani: Majina Yake, Nguvu Yake, Tabia Yake, n.k. Sifa na utukufu ni vinamhusu Mungu peke Yake.

Soma: Isaya 6:5 na 1 Yohana 1:9
Tunapomsifu Mungu kwa sababu ya vile alivyo na kupata uelewa wa kina wa utakatifu Wake wa kutisha, tunagundua hali yetu ya dhambi kwa namna mpya. Tunapaswa kufanya nini na uelewa wetu wa hali yetu ya dhambi? (Ungama dhambi zako na pata msamaha na utakaso wako katika Yesu.)

Soma: Mathayo 7:7, 8
Yesu anatualika kufanya nini? Anahidi nini?

(Yesu anatualika kuomba, lakini siyo kuomba tu. Anatutaka tutafute na kubisha mlango. Hili huonesha ongezeko la shauku, shughuli, na juhudi katika maombi. Tunapoomba bila kuchoka, tukiomba katika jina Lake na kulingana na mapenzi Yake, anaahidi kujibu. Tazama Yohana 14:14 na 1 Yohana 5:14.)

Soma: Yohana 6:37
Je, Yesu anaweza kutufukuza tukimwendea? (Kamwe! Ikiwa una njaa na kiu ya kuwa Naye zaidi, haijalishi hali uliyonayo au mazingira uliyomo, atakukaribisha kwa mikono iliyonyooshwa. Yeye anasema tu, "Njoo!")

> "Hakuna hatari yo yote kuwa Bwana atapuuza maombi ya watu Wake. Hatari ni kuwa katika majaribu na vikwazo watakakatishwa tamaa, na kushindwa kuomba" (Christ's Object Lessons, uk. 175. 1).

Kila siku, tafuta picha mpya ya Yesu katika Neno la Mungu lililoandikwa. Omba na tumia kile unachokigundua katika namna unavyoishi na jinsi unavyomwabudu. Chukua ahadi za Mungu na zifanye kuwa za kwako na ziombee, ukizitumia katika mahitaji yako ya kila siku. Neno la Mungu halikusudiwi kusomwa tu; limekusudiwa pia kufanywa maombi.

Kujifunza jinsi ya kuanza kuomba Neno, tembelea: https://bit.ly/PrayingThePromises. Au skani kodi hii ya QR kwa kutumia kamera ya simu yako!

SHUGHULI YA KIMYA-KIMYA

1. Weka kipima muda kwa dakika moja na kaa kimya, ukisubiri kipige kengele bila kuangalia saa ya ukutani.
2. Baadaye, jiulize ni kwa muda gani dakika hiyo ilihisiwa. Ilionekana kama umilele? Ilikuwa jambo baya kukaa kimya kwa muda wote huo?
3. Ndiyo, sisi wanadamu hatuhusiani vizuri sana na ukimya.

Tunahisi hitaji la "kujaza" nafasi tupu kwa muziki, kujishughulisha, kupitia jumbe zetu za simu na mitandao ya kijamii, na kelele. Lakini Mungu anatuita tutoke katika makelele hayo, asubuhi na mapema wakati vitu vyote bado viko kimya, tuwe kimya na kumngoja Yeye. (Tazama Zaburi 46:10 na Zaburi 25:4, 5.)

4. Tunapomngoja wakati tunapokuwa tukisoma Neno Lake na maombi, tutaona kwa uwazi zaidi picha za Yesu na jinsi alivyo, na mioyo yetu itapata shauku kwa ajili Yake zaidi na zaidi.

JIZOEZE

1. Mpe kila mmoja dakika saba:
   a. Aombe kwa ajili ya Roho Mtakatifu amfunulie picha mpya ya Yesu katika Neno la Mungu.
   b. Soma Mathayo 14:13–21. Tafuta picha mpya ya Yesu.
2. Mpe kila mmoja dakika saba aombe na kusoma hiyo aya tena. Mwulize Mungu kile anachotaka ukitumie kutoka katika ayah ii kwa maisha yako sana.
3. Mpe kila mmoja dakika saba aeleze yale aliyoyagundua na kuyaelewa wakiwa katika makundi ya watu wawili wawili.

Alika wote walioshawishika kuwa uhusiano wa kina zaidi na Mungu katika Neno Lake na wafanye maombi wakiwa wamepiga magoti.

Ombi: "Mpendwa Baba Mungu, tusamehe kwa nyakati ambazo tulipoteza mwelekeo sahihi wa kumtafuta Mwanao katika Neno Lako. Tusaidie tumwone Yesu katika Neno Lako kilsa siku na kutumia kile tunachokisoma kwa ajili ya maisha yetu. Yafanye maisha yetu ya maombi kuwa ya kina zaidi ili yawe yanayotoa uzima, maongezi yenye maana katika nyakati zetu! Katika jina la Yesu, amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 3

Kila siku, kwa moyo wa maombi, tafuta picha mpya ya Yesu katika Neno la Mungu. Mwombe Mungu akuguse kwa kile unachopaswa kukitumia katika maisha yako kwa siku ile. Ishi kwa kufuata ulichojifunza!

Kwa ajili ya kujifunza kwa kina zaidi, durusu maisha ya Yusufu: Mwanzo 37–47. Unapofanya hivyo, jiulize, "Ni kwa jinsi gani kisa cha Yusufu kinatupatia picha mpya za Yesu?" Kuna matukio mengi ya usambamba. (Soma Patriarchs and Prophets, uk. 239, kuona baadhi ya mifano.)

Somo jingine lenye utajiri linapatikana kwa kusoma kitabu chote cha Ufunuo ukiwa na lengo moja: kupata picha mpya za Yesu! Utashangaa kwa kile utakachokigundua!

Kutafuta njia mpya na zenye maana kuhusiana na jinsi ya kusoma na kujifunza Neno la Mungu? Soma Kiambatanisho 7, "Funguo za Kupata Uzoefu wa Neno la Mungu."

# Kila Siku...
# Pokea Ubatizo Mpya wa Roho Mtakatifu

Unatamani ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu kila siku? Unauombea mahsusi kwa ajili ya ubaatizo huo? Unaweza kuupata!

> "Sihi kwa ajili ya Roho Mtakatifu. Mungu anasimama nyuma ya kila ahadi aliyoitoa. Ukiwa na Biblia mikononi mwako sema, nimefanya kama ulivyosema. Naleta ahadi Yako, 'Ombeni, nanyi mtapewa; tafuteni, nanyi mtaona; bisheni, nanyi mtafunguliwa'" (Christ's Object Lessons, uk. 147).

> "Hakuna kitu ambacho Shetani anakiogopa sana kama kuwa watu wa Mungu wanafungua njia kwa kuondoa kila kikwazo, na kumwezesha Bwana kumwaga Roho wake juu ya kanisa dhaifu na mkutano usiotubu" (Review & Herald, March 22, 1887, par. 7).

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapojiandaa kufundisha) somo hili la Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu auchunguze moyo wako (Zab. 139:23, 24, Isa. 59:1, 2) na uondoe vizuizi vyote ili aweze kumtuma Roho Mtakatifu akubatize upya kila siku. Omba akupatie njaa ya ubatizo leo na kila siku.

Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo

JALI

1. Katika kikundi chenu kidogo uliza: Ni jambo gani unalolipenda ambalo limetokea wiki hii?
2. Hebu tudurusu Kanuni za Kurudi Madhabahuni:
    - Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo!

- Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana!
    - Sehemu I:  Mwombe Mungu akuamshe kila asubuhi ili uwe na muda usio na haraka pamoja Naye.
    - Sehemu II: Kila asubuhi, iwe kipaumbele chako cha kwanza kutafakari juu ya vile Yesu alivyo na kile ambacho amekifanya kwa ajili yako. Halafu salimisha vyote ulivyo, na vyote ulivyo navyo, na hata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.
    - Sehemu III: Kwa nguvu ya Yesu aishiye ndani yako kwa imani, fuata uongozi Wake katika chaguzi zako zote siku nzima.
- Kanuni 3: Mgundue Yesu katika Neno Lake na Maombi.

3. Ulifanyaje kuhusiana na Kanuni 3 ya wiki iliyopita? (Changamoto: Kila siku kwa maombi mengi tafuta picha mpya ya Yesu katika Neno Lake. Ulipaswa kumwomba Mungu akuoneshe kile ambacho ungekitumia katika maisha yako kwa siku ile na kuishi kulingana nacho.)
4. Ungana na mtu mwingine. Uliza: "Mungu alikusaidiaje kuiishi changamoto ya wiki iliyopita?" Wapatie vikundi vya watu wawili wawili dakika kati 2-3 za kujadili pamoja. Baadaye, uliza ikiwa kuna mtu yeyote angependa kueleza kile ambacho Mungu alikifanya katika maisha yake alipoikubali changamoto.

UNGANISHA

1. Kusanyikeni katika timu za watu wawili wawili. Kila timu ina dakika tano za kutumia aina zozote za vifaa walivyo navyo kuonesha kwa njia ya vielelezo maana ya "kuzamishwa kabisa." Watie moyo wawaoneshe wanatimu wa vikundi vingine vya watu wawili wawili.
2. Uzoefu huu unahusianaje na Roho Mtakatifu? Kama waumini leo, unaweza kusema tumezamishwa kabisa katika Roho Mtakatifu? Ni kwa nini tumezamishwa au ni kwa nini hatujazamishwa?

Leo tutachunguza maana ya kuomba na kupokea ubatizo wa kila siku wa Roho Mtakatifu.

GUNDUA

Omba: "Baba mpendwa uliye mbinguni, tuletee kiu ya ubatizo wa Roho Mtakatifu. Tafadhali mtume Roho Mtakatifu atufundishe kuhusu Karama hii. Katika jina la Yesu, amina."

## Tunawezaje Kubatizwa na Roho Mtakatifu?

Viongozi: Mwelekeze kila mtu afanye kazi katika kikundi chake. Elekeza vikundi vyote wachunguze aya hizi nne na wajibu swali, "Hatua tano za kubatizwa na Roho Mtakatifu kila siku ni zipi?"

Yohana 7:37–39

Hatua 1: Njoo kwa Yesu ukiwa na kiu na umwamini.

Matendo 2:38

Hatua 2: Tubu.

Hatua 3: Batizwa kwa maji.

Matendo 5:32

Hatua 4: Mtii Mungu.

> Utii ni kipimo cha uanafunzi. Ni kuzitunza amri kunakothibitisha udhati wa madai yetu ya upendo. Wakati fundisho tunalolikubali linapoua dhambi moyoni, linaposafisha uchafu kutoka rohoni, linapozaa tunda la utakatifu, tunaweza kujua kuwa ni ukweli wa Mungu (Thoughts from the Mount of Blessings, uk. 146).

Luka 11:13

Hatua 5: Mwombe Mungu Baba akupatie Zawadi hii.

Katika Christ's Object Lessons, tunapata maelezo yafuatayo kumhusu Yesu akiwa duniani:

> Siyo kwa ajili Yake Mwenyewe, bali kwa ajili ya wengine, aliishi na alifikiri na aliomba. Kutoka katika saa alizozitumia akiwa na Mungu alitoka kila asubuhi kuwaletea watu nuru ya mbinguni. Kila siku alipokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu (Christ's Object Lessons, uk. 139, italiki imeongezwa).

O, ni muhimu kiasi gani mioyo yetu inapaswa kusukumwa kujua kuwa Yesu Mwenyewe alipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu! Kwa kuwa alihitaji Zawadi hii, kwa uzito kiasi gani sisi tunahitaji Zawadi hii kila wakati wa maisha yetu!

Kuna mambo mawili makubwa yanayotokana na ubatizo wa Roho Mtakatifu:

- Tunapokea tunda la Roho Mtakatifu (Wagalatia 5:22, 23).
- Tunapokea nguvu ya kuwa shahUidi wa Kristo (Matendo 1:8).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu hutubadilisha ndani kutupatia tabia ya Kristo na hutubadilisha nje tuwe ushahidi wa Kristo katika yote tunayoyasema na kuyafanya. Mungu Baba ni Mtoaji wa vipawa vyote vilivyo vyema na anafurahia sana anapotupatia Zawadi ya Roho Mtakatifu kila siku.

SHUGHULI
Hapa tutatoa kielelezo cha Ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Vifaa Vinavyohitajika: bakuli/beseni kubwa, sponji kubwa, jiwe kubwa, na ndoo mbili (au tatu) kubwa za maji, na kikombe kidogo cha plastiki au glasi ya kunywea maji.

Kielelezo cha Moyo Laini

- Mwaga maji juu ya jiwe kubwa. Sema: "Ikiwa tuna moyo mgumu—wa jiwe—hatuwezi kufyonza maji ya Roho Mtakatifu. Mambo kama kiburi, uchungu, na hasira huifanya mioyo yetu kuwa migumu."

- Soma Ezekieli 36:26, 27: "Nami nitawapa ninyi moyo mpya, nami nitatia roho mpya ndani yenu, nami nitatoa moyo wa jiwe uliomo ndani ya mwili wenu, nami nitawapa moyo wa nyama. Nami nitatia roho yangu ndani yenu, na kuwaendesha katika sheria zangu, nanyi mtazishika hukumu zangu, na kuzitenda."
- Mwaga maji juu ya sponji na sema: "Mungu atatupatia moyo mpya na Roho mpya, na moyo wetu utakuwa kama sponji ambalo linaweza kumfyonza Roho ambaye atabadili njia zetu. Na anaweza kutiririka (kukamuliwa) kutoka ndani yetu, kwa hiyo tunafanana na Yesu katika mahusiano yetu na wengine."
- Onesha jinsi ambavyo ni rahisi kwa Roho Mtakatifu anaweza "kukamuliwa nje" kwa wengine wakati tunapokuwa na moyo "laini" wa nyama.

Kielelezo cha Kujaa Mpaka Kufurika

- Kuendeleza kielelezo kilichotangulia, shikilia kikombe juu ya bakuli/beseni kubwa. Sema: "Kikombe hiki ni sisi. Kinaonekana kuwa kizuri, lakini kina faida gani ikiwa hakina kitu ndani yake?"
- Mwombe mtu mmoja ajaze kikombe nusu kwa maji. Uliza: "Je, hiki ndicho kiasi cha Roho Mtakatifu tunachokihitaji?" (Hapana!) Jaza hadi 3/4 ya kikombe na uliza swali hilo hilo. (Hapana!)
- Uliza: Ni kiasi gani cha moyo wetu tunataka kijazwe na Roho Mtakatifu? (Moyo wote!)
- Mwambie yule aendelee kumwaga polepole, na kuyafanya yajaze glasi na kumwagika katika bakuli/beseni. Sema: "Wakati tunapokuwa tumejazwa Roho hadi kumwagika, hana njia nyingine isipokuwa kuwamwagikia katika maisha ya watu wengine walio katika uwanja wetu wa mvuto."
- Acha kumwaga, halafu uliza: "Lakini tunaridhika kufurika mara moja tu?"
- Endelea kumwaga maji tena, ukitumia ndoo ya kwanza. "Hapna, tunahitaji kuendelea kuomba ili kupewa ZAIDI."
- Anza kumwaga kutoka katika ndoo ya pili. "Je, kuna wakati wowote tunaweza kuacha kuomba kwa ajili ya

ubatizo wa mafuriko haya ya kila siku?" (Hapana!)
- Endelea kumwaga! "Usisahau kuomba kila siku kwa ajili ya ubatizo wa Roho Mtakatifu ili mwe mashahidi wenye ufanisi kwa ajili Yake, daima mkifurika kwa wingi ili kutoa kwa ajili ya utukufu Wake!"

Toa Ushuhuda Binafsi: Kiongozi, ikiwa una muda mfupi (akika 5–10), ushuhuda binafsi kuhusu jinsi Mungu alivyoubadili moyo wako ngumu na kuufanya uwe mlaini, uutoe kwa wakati huu. (Ikiwa huna uhakika na kile unachopaswa kutoa kama ushuhuda, tazama Kiambatanisho 2.)

JIZOEZE
Mpe kila mtu dakika tano za kuombea hatua zote tano za kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu.

1. Njoo kwa Yesu ukiwa na kiu na umwamini.
2. Tubu.
3. Batizwa kwa maji.
4. Mtii Mungu.
5. Mwombe Mungu Baba kwa ajili ya Zawadi hii.

Uliza: "Kuna jambo lo lote unahitaji kulifanya ambalo hujalifanya, ili uweze kupokea kikamilifu zawadi hii?"

> "Je, tutapigana mieleka na Mungu katika maombi? Je, tutapokea ubatizo wa Roho Mtakatifu? Hili ndilo tunalolihitaji na tunaweza kuwa nalo wakati huu. Ikiwa tutatembea kwa unyenyekevu na Mungu, Mungu atatembea na sisi" (Prayer, uk. 87).

Omba: "Baba mpendwa wa mbinguni, tusamehe kwa kutokuwa na shauku ya kupata Zawadi uliyoiahidi. Tusaidie kuomba na kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu kila siku. Badilisha mioyo yetu ili tuwe na tabia ya upendo ya Yesu. Tufanye kuwa mashahidi wasio na hofu wa Yesu. Katika jina la Yesu, amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 4
Kila siku omba na pokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu. Jizoeze kupokea Zawadi hii kwa imani, siyo kwa hisia. Fuata uongozi Wake. Na endelea kuomba ili upate zaidi na zaidi!

> Wote wanaoweka jisalimisha na kuweka wakfu moyo, mwili, na roho kwa Mungu watapokea daima zawadi mpya ya nguvu ya mwili na akili. Mgao usioisha wa mbinguni upo kwa ajili yao. Kristo huwapa pumsi ya roho Yake Mwenyewe, uzima wa uzima Wake Mwenyewe. Roho Mtakatifu huleta nguvu za juu sana ili zifanye kazi katika moyo na akili. Kwa ushirikiano na Kristo, wanakamilika ndani Yake, na katika udhaifu wao wa kibinadamu wanawezeshwa kufanya matendo ya Yeye Mwenye Nguvu Zote (The Desire of Ages, uk. 827).

## Kila Siku…
# Penda Familia Yako Kwa Kujitoa Mhanga

Imeandikwa hivi kuhusu Yohana Mbatizaji: "Naye atatangulia mbele zake katika roho ya Eliya, na nguvu zake, ili kuigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na kuwatilia waasi akili za wenye haki, na kumwekea Bwana tayari watu waliotengenezwa" (Luka 1:17).

## Ushuhuda wa Mwandishi

Mwaka 1999, wakati wa usiku wenye baridi katika jiji la Michigan, nilisikia wito wa Eliya kurudisha moyo wangu kwa watoto wangu. Sikusikia wito huu kupitia kwa hubiri lililohubiriwa kutoka katika mimbari au kutoka katika sura ya kitabu. Nilisikia wito wa Eliya kupitia kwa vilio vya watoto wangu.

Nilikuwa nilikusanya karatasi zangu na brifukesi yangu ili nitoke nje na kukimbia kuelekea kwenye mkutano wa kupanga ujenzi wa jengo kubwa la kanisa. Nilikuwa na haraka. Watoto wangu, Jason na Julie, walikuwa na umri wa miaka 6 na 3. Walinisikia nikijiandaa kuondoka. Walinikimbilia, wakiniuliza maswali, "Unaenda wapi, Baba?"

"Naendea kwenye mkutano," Nilijibu kwa kusema ukweli wenyewe ulivyokuwa.

"Baba, kaa nyumbani usiku huu!" walijibu. "Kila siku unaondoka! Baba, huchezi nasi tena!"

Niliinama kuwakumbatia na kuwakumbatia mwanangu na binti yangu haraka haraka. Mikono yao midogo midogo ilinifunga na kunibana shingoni kwa nguvu nyingi. Nilipojaribu kuinuka, hawakuniruhusu niende! Walining'ang'ania kwa nguvu zao zote. Walikuwa wakijaribu kumbana baba yao aliyeipenda kazi yake kupita kiasi abaki nyumbani.

Ilibidi kubandua pole pole mikono yao kutoka katika shingo yangu ili niende. Walianza kulia. “Baba, usiku huu tu! Tafadhali kaa nyumbani!”

Nilitoka nje ya nyumba kwa nguvu na kufunga mlango. Nilipokuwa nikitembea katika theluji, picha ya wanangu wakinililia na kuniita iliendelea kubaki na kuweka uzito katika moyo wangu. Nilipokuwa nikitembea katikati ya theluji kuelekea katika mkutano wa kanisa, Mungu aliongea na moyo wangu. Aliniita kwa jina. Nilisita kuendelea na safari. Usiku ule, theluji ikiniangukia kila upande, Mungu aliniita nirudi nyumbani kwa watoto wangu. Kwanza aliongea na mimi kupitia vilio na upendo wa watoto wangu: “Baba, kaa nyumbani!”

Ule ulikuwa wito mgumu kwangu. Kila siku kwa siku saba nilikuwa nje usiku kwa wiki nzima, nikiwasaidia wengine wakati napuuza watoto wangu mwenyewe. Ulikuwa wito ulioniumiza wa rehema ulioleta uponyaji kati yangu mimi, Jason, na Julie.

Tangu siku ile na siku zilizofuata, nilianza kusema hapana kwa maombi mengi ili niweze kusema ndiyo kwa familia yangu. Haikuwa rahisi! Mungu alinisaidia kuanza kulinda muda kwa ajili ya kila mtoto, na kwa ajili ya mke wangu, Aprili, na tuliweka vipaumbele vya muda tukiwa pamoja.

Mwanzoni, watoto wangu hawakuwa na shauku ya kutumia muda nami. Nilikuwa nimesema hapana kwa maombi yao mengi. Mara nyingi, nilijihisi kama nashindwa. Lakini wito wa Eliya unakuja ukiwa na nguvu ya uponyaji kutoka kwa Bwana. Bwana aliwasaidia watoto wangu kunisamahe. Hakika nilishuhudia akiurudisha moyo wangu kwao na mioyo yao midogo ikirudishwa kwangu. Mungu asifiwe!

Yohana, akiwa na Roho Mtakatifu yule yule wa Eliya, aliwaandaa watu kwa ajili ya ujio wa Masihi. Kama Eliya, Yohana alitoa wito kwa ajili ya uamsho. Alihubiri, “Tubuni, kwa kuwa ufalme wa mbinguni umekaribia” (Mathayo 3:2).

Yohana, kama Eliya, aliita mioyo ya akina baba iwarudie watoto wao. Leo, tumeagizwa kufanya hivyo vivyo hivyo.

Yohana aliwaandaa watu wa karne ya kwanza kumpokea Yesu kama Masihi. Leo, tumeitwa kuwandaa watu kwa ajili ya kumpokea Yesu kama Mfalme wa wafalme atakayekuja katika mawingu!

Kuiponya familia ni sehemu kiini cha uamsho, na sehemu ya kiini cha kurudi madhabahuni. Uamsho unapaswa kuwa mdundo wa moyo wa kila siku wa nyumba zetu. Ibada kwenye madhabahu kama familia inapaswa kuwa mdundo wa nyumba zetu. Wakati familia zetu zinapopata uzoefu wa uamsho wa kila siku pamoja na Yesu kwa njia ya ibada, muda katika Neno Lake lililoandikwa, na maombi, Roho wa Mungu anatuandaa kwa ajili ya kumpokea Yesu upesi! Sasa ni wakati wa kuuishi ujumbe wa Eliya kwa ajili ya siku hizi za mwisho!

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapofundisha) kanuni hii ya Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu akupe macho mapya ya kuona mahitaji ya wanafamilia wa familia yako. Omba kuwa akuoneshe jinsi ya kuwapenda kumtumikia kila mwanafamilia kwa makusudi na kwa kujitoa mhanga na namana ya kuwaita, pamoja na wewe, kurudi katika madhabahu ya ibada ya kila siku.

<u>Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo</u>

JALI

1. Uliza kikundi: Fikiria wimbo unaoelezea vizuri wiki yako na kwa nini. Shiriki kichwa cha habari cha wimbo huo na kikundi.
2. Uliza: "Zipi ni kanuni za Kurudi Madhabahuni hadi hapa?"
    - Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo!
    - Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana!
        - <u>Sehemu I</u>: Mwombe Mungu akuamshe kila asubuhi ili uwe na muda usiokuwa na haraka pamoja Naye.
        - <u>Sehemu II</u>: Kila asubuhi, iwe kipaumbele chako cha kwanza kutafakari kwa makini juu ya Yesu ni nani na kile ambacho amekifanya kwako. Halafu salimisha vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, na hata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.
        - <u>Sehemu III</u>: Kwa nguvu ya Yesu anayeishi ndani

yako kwa imani, fuata uongozi Wake katika chaguzi zako zote katika siku nzima.

- Kanuni 3: Mgundue Yesu katika Neno Lake na Maombi.
- Kanuni 4: Omba na pokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu.

3. Shirikiana na mtu mwingine. Uliza: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusaidia kuiishi changamoto ya wiki iliyopita, ukiomba na kupokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu?" Wapatie watu katika vikundi vya watu wawili wawili dakika 2–3 wajadiliane. Uliza kundi kubwa ikiwa kuna mtu yeyote anayependa kushiriki na wengine kile ambacho Mungu amemtendea katika maisha yake alipoipokea changamoto.

UNGANISHA

1. Wapange wote katika vikundi vya watu wawili wawili. Waulizane wao kwa wao: "Ni kumbukumbu ipi ya kifamilia ambayo unaipenda zaidi na kwa nini?"
2. Ni vipengele gani hufanya kumbukumbu nzuri ya kifamilia? Ni jambo gani Mungu angependa kulifanya pamoja na familia zetu kabla Yesu hajarudi kutuchukua wote na kutupeleka nyumbani?

Leo tutachanguza jinsi ya kuipenda familia yetu kwa kujitoa mhanga.

GUNDUA

Omba: "Baba Mungu mpendwa, asante kwa ajili ya familia zetu. Tunaona upendo mkubwa na chuki kubwa katika familia zetu. Asante kwa kuwa Mponyaji wa kila maumivu. Fungua mioyo yetu ili ipokee kile Roho Mtakatifu anachotufundisha kwa njia ya Neno Lako. Katika jina la Yesu, amina."

## Jinsi ya Kuipenda Familia kwa Kujitoa Mhanga

Soma: Warumi 13:8
Omba: Ni deni gani kila mtu anapaswa kuwa nalo? (Msidaiwe kitu chochote isipokuwa kupendana.)

Soma: Waefeso 4:29–32
Uliza: Ni chujio gani tunapaswa kulitumia kuchuja maongezi yetu yote? (Zungumza yale tu yanayojenga.)

Uliza: Inatupasa kufanya nini kuhusiana na chuki na uchungu? (Ondoa uchungu wote.)

Uliza: Ni kwa kiwango gani tunapaswa kusameheana? (Msameheane kama Kristo alivyowasamehe.)

Soma: Mathayo 5:23, 24
Uliza: Tunawezaje kutumia aya hii kwa muda wetu wa ibada ya mtu binafsi au ya kifamilia? (Tafuta mapatano kabla ya ibada, ikiwezekana. Ikiwa umeongea na kwa ukali na mwenzi wako au watoto wako au umefanya jambo ambalo limejeruhi wanafamilia, mioyo ya wanafamilia haitakuwa nawe katika ibada. Lakini, ikiwa umeomba msamaha na umetafuta kusahihisha makosa yoyote, kabla ya kuanza ibada, kutakuwa na uwezekano mkubwa wa kukubali uongozi wako.)

Soma: Waefeso 6:12
Uliza: Tunapambana na nani hasa tunapokuwa na migogoro katika nyumba na familia zetu? (Tunapigana vita dhidi ya nguvu za kiroho na uovu wa anga za juu. Ikiwa tunatambua adui yetu wa kweli ni nani—siyo kila mmoja dhidi ya mwenzake—na kumbuka kuwa sisi na familia zetu tunasimama upande wa ushindi, kutakuwa na tofauti kubwa kutusaidia kusamehe na kusuluhisha migogoro.)

Uliza: Unafanya nini ikiwa hujisikii kumsamehe mtu fulani katika familia yako?

Soma: Ezekieli 36:26, 27
Uliza: Ni nani hufanya upasuaji huu wa moyo—wewe au mtu fulani mwingine? Mungu amekupatia ahadi ngapi katika aya hii? (Mungu hufanya upasuaji huu. Yeye peke Yake ndiye anaweza kuufanya! Anatoa ahadi 6–9 katika aya hii, kutegemeana na tafsiri ya Biblia unayoisoma.)

Mwombe Mungu afanye upasuaji wa moyo wako ili aondoa uchungu dhidi ya mtu yule mahsusi. Mwombe Mungu akuondolee kabisa uchungu. Mwombe Mungu akupe moyo mpya wa upendo na msamaha na aufurikishe moyo wako kwa Roho Mtakatifu.

Soma: Waefeso 5:21–33
Uliza: Ni kwa jinsi gani aya ya 21 ni ufunguo kwa ndoa inayofanana na ya Kristo? (Jisalimishe mmoja kwa mwingine kwa ajili ya kicho kwa ajili ya Kristo. Ushauri huu hutoa muktadha kwa ajili ya ushauri wote uliobaki. Ikiwa utafuatwa, tamaa yote kwa ajili ya ukuu wa mtu mmoja juu ya mwingine utasalimishwa kwa Kristo!)

Uliza: Mungu anatoa ushauri gani kwa wake katika aya ya 22–24? Aya ya 33 hutoa muhtasari gani? (Mpende mume wako kwa heshima.)

Uliza: Mungu anatoa ushauri gani kwa waume katika aya ya 25–29? Ni kwa jinsi gani aya 25 hutoa muhtasari wa dhima ya mume? (Mpende mke wako kwa kujitoa mhanda, kama Kristo alivyolipenda kanisa na kujitoa kwa ajili yake.)

Soma: Malaki 4:5, 6
Uliza: Ni ahadi gani mbili Mungu anawapa wazazi na watoto katika siku za mwisho? (Mungu atageuza mioyo ya akina baba [wazazi] iwaelekee watoto wao na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao [wazazi wao]. Sehemu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya siku za mwisho ni kuwa mahusiano ya kifamilia yarejeshwe.)

Kujinyeyekesha mbele za Mungu ili arejeshe mioyo yetu pamoja na watoto na wazazi wetu kunatakiwa kutokee kabla

hatujawa sehemu ya kielelezo cha vizazi vipya kwa ajili ya Kristo.

## Fundisha na Ongelea kuhusu Neno la Mungu!

Soma: Kumbukumbu la Torati 6:4–6
Uliza: Ni kwa namna gani aya ya 4–6 hutuita kupata uzoefu wa uamsho pamoja na Mungu? (Mungu hutuita kumpenda Bwana Mungu wetu kwa mioyo yetu yote.)

Wakati Mungu anapofanya uamsho huu katika mioyo yetu, tunakuwa tayari kwa ajili ya ushauri Wake katika aya ya 7.

Soma: Kumbukumbu la Torati 6:7–9
Uliza: Ni nani anapaswa kuwafundisha watoto wetu? (Wazazi, fundisheni Neno la Mungu kwa "wana wenu"—watoto wenu.)

Uliza: Ni kwa njia gani wazazi wanapaswa kuwafundisha/kuwafanya kuwa wanafunzi watoto wao?

"Uketipo kati nyumba yenu."
Uliza: Ni wakati gani wazazi na watoto wanakaa pamoja? (Kutembea kwenda shuleni, kanisani, wakila chakula, wakiangalia video, wakicheza mchezo, wakifanya kazi kwa kutumia stadi au mradi, n.k.)

"Utembeapo njiani."
Uliza: Ni wakati gani wazazi na watoto hutembea pamoja? (Kununua vyakula, kutembea kutoka katika gari au kwenda kituo cha basi, kutembea umbali mrefu, wakifanya kazi katika bustani au kiwanja, kufagia nyumba.)

"Ulalapo."
Uliza: Ni maongezi gani kumhusu Kristo unaweza kuwa nayo na watoto wako kabla ya kulala? (Labda waulize kuhusu siku yao ilikuwaje. Ni sehemu gani ya siku ilikuwa nzuri zaidi kwao? Ni sehemu gani ya siku ilikuwa mbaya zaidi kwao? Waulize jinsi unavyoweza kuwaombea.)

“Uondokapo.”
Uliza: Ni maongezi gani kumhusu Kristo unaweza kuwa nayo na watoto wako wanapoianza siku? Unawezaje kuifanya ibada ya familia kuwa na mvuto zaidi na shirikishi? (Tazama Kiambatanisho 3 kwa ajili ya ibada za familia zenye ubunifu.)

Tafuta njia za kuonesha mfano kwa watoto wako jinsi ya:

- Kuja kwa Yesu kama ulivyo.
- Kumwabudu Yesu na kumtukuza.
- Kujisalimisha kwa Yesu kama Bwana kuwa kitu cha kwanza asubuhi.
- Kumtafuta Yesu katika Neno la Mungu na katika maombi.
- Kutumia Neno la Mungu kwa maisha yako.
- Kuomba kwa ajili ya kupokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu.

Usisahau kuomba mbaraka kwa ajili ya watoto wako kila siku.

## Funga Neno la Mungu katika Matendo na Mawazo Yako

Kuendelea na Kumbukumbu la Torati 6:7–9:

“Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako.”
Uliza: Unafikiri ni nini maana ya kuwa na Neno la Mungu juu ya mikono yako? (Matendo yetu yanapaswa kupatana na Neno la Mungu.)

“Nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako.”
Uliza: Unafikiri ni nini maana ya kuwa na Neno la Mungu juu ya kipaji cha uso wako? (Mawazo na mitazamo yetu inapaswa kupatana na Neno la Mungu.)

## Lifanye Neno la Mungu kuwa Ukaribisho na Ushuhuda wa Mlango Wako wa Mbele

“Yaandike juu ya miimo ya nyumba yako.”

Uliza: Unawezaje kulifanya Neno la Mungu kuwa “ukaribisho na ushuhuda” kwa wote wanaokuja nyumbani kwako? (Mfano mmojawapo unaowezekana: Weka ahadi moja ya Biblia juu ya mlango kwa ndani. Kwa maombi mengi weka ahadi za Biblia katika vyumba mbalimbali vya nyumba yako, ukilinganisha aya na shughuli zinazoweza kutokea katika vyumba hivyo,  n.k. Ukitumia chaki zisizofutika kwa maji, andika aya ya Biblia katika kioo cha bafuni.)

## Lifanye Neno la Mungu kuwa Ukaribisho na Ushuhuda wa Njia ya Kuingilia katika Kiwanja Chako

“Yaandike juu ya … malango yako.”

Uliza: Unaweza kufanya nini ili kulifanya Neno la Mungu kuwa ukaribisho na ushuhuda wa kiwanja chako? (Alika wageni wako wajiunge na wewe katika matembezi ya maombi ya Bibblia katika kiwanja chako. Ikiwa huna kiwanja kikubwa au unaishi mahali ambapo haiwezekani kufanya matembezi ya maombi ya Biblia katika vitu vya asili, tembelea katika maeneo yaliyo jirani na kuwaombea majirani zako—na waeleze kuwa unawaombea. Uliza, inapowezekana, jinsi unavyoweza kuwaombea.)

Kwa ajili ya mawazo ya matembezi ya maombi ya Biblia tazama kitabu Meet Jesus Outside: Bible Prayer Walks, downloadable for  free at indisicpleship.org.

Je, kuipenda familia ni vigumu nyakati zingine? Mungu daima ana upendo wa kutosha wa kumwaga kupitia kwa wanafamilia ambao si wepesi kuwapenda au kuwasamehe. Mungu ni msamaha wetu kwa watu wasiosameheka

katika maisha yetu. Mungu ni uponyaji wetu wa kurejesha mahusiano ya ndoa na familia zetu ambayo mwanadamu peke yake asingeweza kamwe kuwa na nguvu ya kuyarejesha!

JIZOEZE

1. Mwombe na mwulize Mungu:
   a. Ni kitu gani mahsusi ambacho kila mtu miongoni wanafamilia walio karibu yangu anakihitaji kutoka kwangu ili ajue kuwa nampenda?
   b. Ni nani katika familia yangu anahitaji msamaha au anahitaji nimwombe msamaha?
   c. Ni hatua gani inayofuata?

2. Sikiliza na amini kile ambacho Mungu anakuahidi: "Aa! Bwana MUNGU, tazama, wewe umeziumba mbingu na nchi, kwa uweza wako mkuu na kwa mkono wako ulionyoshwa; hapana neno lililo gumu usiloliweza" (Yer. 32:17).

   "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu.

Fikiria hili …

> Familia moja inayosimamiwa vizuri, yenye nidhamu njema, inanieleza mengi zaidi kuhusu Ukristo kuliko mahubiri yote yanayoweza kuhubiriwa. Familia kama hiyo inatoa ushahidi kuwa wazazi wamefanikiwa katika kufuata maelekezo ya Mungu, na watoto wao watamtumikia Mungu katika kanisa. Mvuto wao unakua; kwa kadiri wanavyotoa, wanapokea ili kutoa tena. Baba na mama wanapata wasaidizi kwa watoto, wanaowapa mafundisho wengine waliyoyapata nyumbani. Majirani wanaoishi nao wanapata msaada kutoka kwao, kwa sababu katikati yao wanatajirishwa kwa muda mfupi na umilele. Familia nzima inaingizwa katika huduma ya Bwana; na kwa njia ya mfano wao wa kicho, wengine

> wanavuviwa wawe waaminifu na wa kweli kwa Mungu katika kushughulikia kundi Lake, kundi Lake zuri.
>
> Ushahidi mkubwa wa nguvu ya Ukristo unaoweza kuwasilishwa kwa ulimwengu ni familia inayosimamiwa vizuri, iliyo na nidhamu njema. Hili litautetea ukweli kuliko kitu kingine cho chote kile kinavyoweza kufanya, kwa kuwa ni ushahaidi hai wa nguvu halisi juu ya moyo (The Adventist Home, uk. 32).

Omba: "Mpendwa Baba Mungu, unapofikiria kuhusu familia zetu, utukumbushe kuwa hakuna jambo lililo gumu Kwako! Unatuambia katika Neno Lako kuwa utatupatia mahitaji yetu yote kulingana na utajiri wako, siyo wetu. Tunasalimisha hofu na wasiwasi zetu pamoja na majeraha yetu Kwako—tukiweka dhamana nafsi zetu na familia zetu katika upendo Wako unaoponya. Tupatie upendo Wako ili tumpende kila mwanafamilia wa familia yetu kama unavyowapenda. Asante kwa kusikia ombi hili. Katika jina la Yesu, amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 5
Chukua hatua inayofuata wiki hii, ukimtumaini Mungu akusaidie kufanya kile ambacho amekusadikisha kukifanya kuipenda familia yako kwa kujitoa mhanga.

## Kila Siku…
# Wafanye Wengine kuwa Wanafunzi wa Yesu

"Unanipenda?" Hilo ni swali ambalo Yesu alimwuliza Petro alipokuwa akimpa agizo lake kama mfanyaji wa wanafunzi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni.

> Swali ambalo Kristo alimwuliza Petro lilikuwa la maana sana. Alitaja sharti moja tu la uanafunzi na huduma. "Unanipenda?" Yesu alisema. Hii ni sifa muhimu. Ingawa Petro angekuwa na kila sifa zingine, lakini bila upendo wa Kristo asingeweza kuwa mchungaji mwaminifu wa kundi la Bwana. Ujuzi, ukarimu, ufasaha, shukurani, na juhudi –vyote ni misaada katika kazi nzuri; lakini pasipo upendo wa Yesu katika moyo, kazi ya mchungaji wa Kikristo ni ni bure (The Desire of Ages, uk. 815.2).

Biblia inatuambia, "Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza. Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii" (Mathayo 22:37–40).

Msingi wa kuwa mfanya wanafunzi wa kweli! Tunapenda kwa sababu alitupenda.

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapojiandaa kufundisha) kanuni ya Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu akupe upendo na unyenyekevu unaouhitaji ili kuhudumu kwa kujitoa mhanga na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi wa Yesu. Kumbuka, Yesu alikuwa tayari kuacha kila kitu na kuja kufa juu ya msalaba kwa ajili ya mtu mmoja ili aende mbinguni.

JALI

1. Swali kwa ajili ya wana kikundi kuulizana: "Ikiwa ungekuwa na kila kitu unachokihitaji sasa hivi, ungeomba nini?"
2. Hebu tupitie kwa ufupi kanuni za Kurudi Madhabahuni:
   - Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo!
   - Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana,
     - Sehemu I: Mwulize Mungu akuamshe kila asubuhi ili uwe na muda usiokuwa na haraka pamoja na Mungu.
     - Sehemu II: Kila asubuhi, iwe kipaumbele chako cha kwanza kutafakari juu ya Yesu alikuwa nani na kile ambacho amekifanya kwa ajili yako. Halafu salimisha vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, na hata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.
     - Sehemu III: Kwa njia ya nguvu ya Yesu anayeishi ndani yako kwa imani, fuata uongozi Wake katika chaguzi zako zote katika siku nzima.
   - Kanuni 3: Mgundue Yesu katika Neno Lake na maombi.
   - Kanuni 4: Omba na pokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu.
   - Kanuni 5: Penda familia yako kwa kudhamiria.
3. Kaa pamoja na mtu mwingine. Uliza: "Ni kwa jinsi gani Mungu alikusudia kuishi changamoto ya wiki iliyopita?" (Changamoto ilikuwa: Chukua hatua inayofuata, ukitumaini kuwa Mungu atakusaidia kufanya yote aliyokusadikisha uyafanye wakati unaofuata ili kuipenda familia yako kwa kudhamiria.)
4. Wapatie watu walio katika vikundi vya watu wawili wawili dakika 2-3 wajadiliane. Uliza kundi kubwa ikiwa mtu yeyote anapenda kushiriki kile ambacho Mungu alimfanyia katika maisha yake baada ya kupokea changamoto.

UNGANISHA

1. Waelekeze watu wote wakae katika vikundi vya watu wawili wawili. Wapatie kila kikundi kitu kidogo ambacho kina kusudi linaloeleweka (mifano: zana, tunda, bibu ya mtoto, kitana, n.k.). Kipe kikundi dakika nne kuonesha

thamani ya kitu hicho, jinsi ya kukitunza, na jinsi ya kukitumia katika namna ambayo inaleta maana na mfundishe mtu mwingine afanye hivyo hivyo.

2. Ni kitu gani mtu fulani alikifanya ambacho ulikiona kufaa na kuwa na msaada kwako, ukakipenda kitu hicho, ukataka kukitumia kitu hicho, na ukatamani kukishiriki na wengine? (Eleza.) Tunajifunza nini kutokana na shughuli hii ambacho tunaweza kukitumia kufanya wanafunzi wa Kristo?

Leo tutachunguza kile ambacho kinamaanisha kuwafanya wengine kuwa wanafunzi wa Yesu.

GUNDUA

Omba: "Baba wa milele, Mwanao Yesu alituita kufanya wanafunzi ulimwenguni kote. Tafadhali mtume Roho Mtakatifu atusaidie kuwa waaminifu kwa wito wetu.Katika jina la Yesu, amina."

Kwa nini inatupasa kukubali wito wa kuwa wafanya wanafunzi?

## Tumeamrishwa Kufanya Wafanya Wanafunzi!

Yesu ana mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo 28:18–20)! Anatuagiza kufanya wanafunzi.

Wanafunzi = Wafanya wanafunzi. Yote mawili lazima yawe kitu kimoja.

Lakini, ikiwa tunataka kuwa wafanya wanafunzi, inatupasa kufuata njia za Yesu, ambaye ni Mfanya Wanafunzi Mkuu.

## Mbinu ya Yesu ya Kufanya Wanafunzi

1. Soma: Luka 6:12–16

   Tumia usiku wa maombi kabla ya kuchagua "wanafunzi kumi na wawili." Kwa maneno mengine, tumia usiku kwa maombi ya kukusudia ukimwomba Mungu akupe wale ambao nawataka wewe uwekeze muda na malezi ya

kuwafanya wanafunzi. (Unajiuliza jinsi ya kutumia usiku wa maombi? Tazama Kiambatanisho 1.)

2. Soma: Mathayo 4:18–20
    a. Nenda na uwatembelee wanafunzi watarajiwa mahali wanapoishi/ wanapofanya kazi.
    b. Waalike wakufuate wewe kama unavyomfuata Yesu, wafanye kazi na wewe wakati unapokuwa ukimfanyia Yesu kazi, na kujiunga na wewe katika kumtumikia Yesu.
    c. Wafundishe wanafunzi wako kuwa wavuvi wa watu.
3. Soma: Marko 3:13, 14 na Mathayo 4:23

    Waalike wanafunzi wako wawe pamoja nawe. Toa muda na fursa, kwa njia ya aina zote tofauti za maisha ya kila siku na shughuli za huduma, kushirikiana nao, ili waone jinsi unavyomfuta Yesu, jinsi unavyoomba, unavyofanya unapokuwa umechoka, jinsi unavyoitikia unaposongwa, na jinsi unavyojifunza Neno la Mungu.

> Ilikuwa kwa njia ya kukutana binafsi na kuchangamana ambapo Yesu aliwafundisha wanafunzi Wake. Nyakati zingine aliwafundisha, akikaa miongoni mwao kando kando ya milima; nayakati zingine kando ya bahari, au akiwa anatembea njiani pamoja nao, alifunua siri za ufalme wa Mungu. Hakuhubiri kama watu wanavyofanya leo. Mahali popote mioyo ilipokuwa wazi kupokea ujumbe wa Kimungu, alifunua kweli za wokovu. Hakuwaamrisha wanafunzi wake kufanya hili au lile, lakini alisema, "Nifuateni Mimi." Katika safari Yake iliyomfanya kupita katika nchi na miji aliienda pamoja nao, ili waone jinsi alivyowafundisha watu. Aliunganisha maslahi yao na ya Kwake, na waliungana Naye katika kazi (The Desire of Ages, uk. 152).

   b. Watume waende kuhubiri na kufundisha, ukiamini kuwa Yeye aliyekuita atawaita na kuwawezesha.

4. Soma: Luka 9:1, 2
   a. Waite wamwombe Mungu ili wapokee nguvu kwa njia ya ubatizo wa Roho Mtakatifu.
   b. Wafundishe kuwa, kwa njia ya jina la Yesu, wana mamlaka juu ya roho wachafu na nguvu za giza.
   c. Wafundishe kuwaombea wagonjwa na kuanganisha na maombi yao ya imani na elimu ya mtindo wa maisha yenye afya na matibabu ya asili kwa ajili ya kutibu magonjwa. (Kwa ajili ya vidokezo vya kiutendaji vya maisha yenye afya, tazama Kiambatanisho 6.)
   d. Watume waende kutangaza ufalme wa Mungu na kuleta uponyaji wa mioyo na roho zinazoumwa dhambi kwa njia ya nguvu ya Neno la Mungu.

Mungu Baba yetu alimfanya Yesu kuwa mwanafunzi alipokuwa duniani. (Tazama Isa. 50:4.) Mungu Baba yetu na Roho Mtakatifu wanapenda na wanawekeza katika kutufanya sisi kuwa wafanyaji wa wanafunzi kama Yesu Mwenyewe alivyofanyiwa.

JIZOEZE

Mchezo wa "Nifanye Mimi Mwanafunzi"

1. Waulize wana kikundi wachukue karatasi zisizokuwa na maandishi yoyote na waandike kanuni moja ya kiroho au ya tabia ambayo wameiongeza katika ratiba yao ya kila siku ya kukuza uhusiano wao na Yesu. Elezea kuwa kanuni au tabia hii inapaswa kuwa:
   - Na maana katika kujenga uhusiano na Yesu
   - Fupi na sahili
   - Inayoweza kuigwa na mtu yeyote
2. Waelekeze washiriki waunde mistari miwili inayoangaliana, umbali wa takribani futi 10 (mita 3) kati ya hiyo mistari miwili. Mistari yote miwili inapaswa kuwa na idadi sawa ya watu.

3. Eleza kwa mistari yote miwili kuwa mtu aliye mbele ya mwenzake ndiye atakuwa mwanafunzi wake katika mchezo.
4. Eleza mandhari: "Kuna shimo lenye kina kirefu cha futi 1,000 (mita 300) kwenda chini linalowatenga ninyi watu wawili. Mungu amekuchagua kumfanya mwenzako ng'ambo ya shimo hili kubwa kuwa mwanafunzi."
5. Waelekeze washiriki kila mmoja kukunja karatasi zao na kuzitupa, baada ya kuhesabu mpaka 10, kwa mwanafunzi wao mtawalia. (Ni muhimu kuwa karatasi hizi zisiangukie katika shimo kubwa linalowatenga. Ikitokea hivyo, timu zote mbili zishirikiane kuziokota karatasi hizi bila yeyote kuingia shimoni.)
6. Sasa hamia katika ufanyaji wanafunzi wa makusudi kati ya wanafunzi hao wawili washirika.
7. Kazia hatua zifuatazo kwa wale ambao itawabidi kubaki pande zote mbili za mstari:
   - Soma maelezo ya mfanya wanafunzi mwenzako yaliyorushiwa kwako.
   - Toa nafasi kwa kila mfanya wanafunzi kueleza kile alichokiandika.
   - Ikiwa maswali yatajitokeza, kila mtu ajibu maswali ya mwenzake.
   - Toa nafasi kwa kila mfanya wanafunzi ampe changamoto mwenzake kufanyia mazoezi kile kilichoandikwa na halafu amwambie, "Tuonane wiki ijayo!"
8. Waelekeze washiriki kila mmoja ageukie upande mwingine kinyume na mwenzake kana kwamba wanatawanyika hadi wiki ijayo na kila mmoja amwombee mwanafunzi wake mtawalia kwamba kila mmoja aweze kufanyia kazi kile walichopewa.
9. Sema: "Wiki moja imepita. Mgeukie mwanafunzi wako tena."
10. Ingia katika mjadala na uliza mistari yote miwili: "Hili shimo kubwa linaweza kuwakilisha nini katika maisha yetu? Ni mambo ya aina gani yanaweza kututenga na mtu yule tunayejaribu kumfanya mwanafunzi?" (Majibu yanayoweza kutolewa: umri, kabila, lugha, hali ya kijamii na kiuchumi, kiwango cha elimu, n..k.)

11. Zoezi la hiari linaloonesha umuhimu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu:
    - Wapatie washiriki kipande kidogo cha sponji na waambie kuwa kipande hiki kinatuwakilisha sisi na ushuhuda wetu. Baada ya kuhesabu mpaka 3, mwambie kila mmoja atupe hicho kipande cha sponji kwa mwenzake. (Hawataweza kwenda mbali!)
    - Halafu, chukua ndoo kadhaa za maji na uruhusu washiriki kuchovya vipande vya sponji ndani ya maji. Baada ya kuhesabu mpaka 3, rudia zoezi. (Vipande vya sponji pengine vitaweza kufika kwa wenzao! Washirika wanaweza kuloana wakati wanapodaka vipande vya sponji.)
    - Maji ni nguvu ya Roho Mtakatifu (rejelea mfano wa Roho Mtakatifu). Nguvu ya Roho Mtakatifu hufanya mchakato wa ufanyaji wanafunzi wetu kuwa na ufanisi.
12. Sema: "Ingawa kuna vikwazo vinavyochimba shimo hilo, Roho Mtakatifu ana shauku ya kujenga daraja kutoka kwangu hadi kwa yeyote ambaye ametuita kumfanya kuwa mwanafunzi. Ombea Roho Mtakatifu ajaze mapengo na kuufanya ushuhuda wako kufanikiwa!" [Tulia kwa ajili ya maombi ya kimya.]
13. Sema: "Chukua koleo ya kufikirika na jaza shimo katikati ya mistari." Baadaye, sema, "Tunapoomba kwa ajili ya msaada Wake, anajaza mapengo yanayotutenga."
14. Sasa shimo kubwa limejazwa, alika wanafunzi wakutane pamoja mmoja kando ya mwingine. Waelekeze washiriki kutumia fikira zao kuuliza na kujibu swali, "Changamoto ya wiki iliyopita ilikwendaje?
15. Waelekeze wapeane shuhuda kuhusu kile walichokiandika na jinsi kilivyoathiri uhusiano wao na Yesu.
16. Waelekeze wawape changamoto wanafunzi wenza tena kufanyia mazoezi kanuni hii na, wakati huu, waombe na mwanafunzi wao.

17. Waelekeze wanafunzi washirika wageukie upande mwingine kuwakilisha muda wa kutengana. Halafu, waelekeze waangaliane tena.
18. Liambie kundi: “Tutachukulia kuwa mmekuwa mkionana kwa wiki kadhaa na kuwa mwanafunzi wako anaelewa, anafanya juhudi binafsi, na anafanyia mazoezi kile ambacho umemwambia. Sasa mpe changamoto mwanafunzi wako, baada ya hapo, kushiriki kile ambacho wamejifunza kutoka kwako na mtu mwingine ndani ya chumba. Zingatia kuwa jinsi unavyowafanya kuwa wanafunzi ndivyo watakavyowafanya wengine kuwa wanafunzi. Kwa hiyo, dhamiria kabisa!”
19. Ruhusu dakika chache kwa ajili ya wafanya wanafunzi kusambaa na kutafuta wanafunzi wenza wa kufundisha kile walichofundishwa. Hili linafanyika kwa njia mbili- kila mmoja akimfundisha mwenzake. Halafu waelekeze waombeane.
20. Mwalike kila wanafunzi atafute mfanya wanafunzi mweza wa awali. Waelekeze kuulizana, “Ilikuwaje uliposhiriki na mtu mwingine kile nilichoshiriki nawe?”
21. Eleza: Baada ya muda, unataka kuona kanuni za uanafunzi unazozifundisha zikitoka:
    - Kutoka kichwa (ufahamu)
    - Kwenda moyoni (shauku)
    - Kwenda mikononi (mazoezi)
    - Kwenda miguuni (kwenda kwa wengine)
22. Alika kila mmoja kuunda timu za watu wane wane. Uliza “Ni kiwango gani cha mchakato huu unakifanya sasa pamoja na wengine?” Baada ya dakika 2–4, omba watu wanaojitolea kushiriki majibu yao kwa swali waliyokuwa wakiyajadili. Tena, thibitisha umuhimu wa mchakato ulioelezwa hapo juu. Shiriki ushuhuda, mfupi, wa kibinafsi ikiwezekana.
23. Waalike washiriki kupiga magoti katika unyenyekevu mbele ya Bwana Yesu.
24. Toa wito: “Ni akina nani wanaotaka kuwa makusudi zaidi katika kuwafanya wengine kuwa wanafunzi? Ni nani anayependa kufanya ombi la usiku au la mchana la kumwomba Mungu ampe mtu wa kumfanya kuwa mwanafunzi? Ikiwa uko tayari kuchukua changamoto hii, piga magoti pamoja nami kwa unyenyekevu mbele ya Bwana Yesu wakati tunapoomba kwa ajili ya kupata nguvu ya kufanya kile ambacho anatuita kukifanya.”

Omba: “Baba mpendwa wa mbinguni, tuna muda mfupi uliobaki wa kufuata amri ya Mwokozi wetu ya kwenda na kuwafanya watu kuwa wanafunzi ulimwengu kote.

Tumewapa wengine taarifa kuhusu Yesu. Utusamehe kwa kutokuwa tayari kulipa gharama inayolipwa kwa ajili ya kufanya wanafunzi. Kufanya wanafunzi hugharimu muda wetu wakati tuna mambo mengi ya kufanya. Inagharimu raha yetu tunapokuwa tumechoka. Inagharimu heshima yetu wakati Roho Mtakatifu anapotutuma kwa mtu ambaye hatutaki kumwona. Ulimgharimu Yesu maisha Yake ili kutengeneza njia ya kurudi katika madhabahu ya kutufanya wanafunzi. Tutumie Roho Mtakatifu atuwezeshe kufanya wanafunzi wa Yesu wanaotembea Naye, wanaozunguza Naye, na mtangaze kwa nguvu ya moyo unaodunda. Katika jina la Yesu, amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 6
Ukusudie kuhusiana na kumfanya mtu kuwa mwanafunzi kwa ajili ya Yesu. Fanya maombi ya "usiku" au wakati maalumu wa maombi kumwomba Mungu kuhusiana na nani anataka umfanye mwanafunzi na jinsi ya kumfanya mwanafunzi. Liweke mbele ya Bwana. Omba, na nenda ushiriki jambo hilo pamoja na mtu yule.

Kumbuka…

> Mbinu ya Kristo pekee itatoa mafanikio ya kweli katika kuwafikia watu. Mwokozi alijichanganya na watu kama yule aliyewatakia mema. Alionesha huruma Yake kwa ajili yao, alihudumia mahitaji yao, na alipata imani yao. Ndipo aliwaita, "Nifuateni Mimi." Kuna hitaji la kuja karibu na watu kwa juhudi binafsi. Ikiwa muda mfupi ungetolewa kwa kutoa mahubiri, na muda mwingi zaidi ungetumiwa katika huduma binafsi, matokeo makubwa zaidi yangeonekana. Maskini inapaswa wasaidiwe, wagonjwa watunzwe, wenye huzuni na waliofiwa wafarijiwe, wasio na maarifa wafundishwe, wasiokuwa na uzoefu washauriwe. Lia na wale wanaolia, na furahi pamoja na wale wanaofurahi.
> Vikiunganishwa na nguvu ya ushawishi, nguvu ya maombi, nguvu ya upendo wa Mungu, kazi hii haitaweza, haiwezi, kutokuwa na matunda (The Ministry of Healing, uk. 143).

## Kila Siku…
# Ishi Utume Wako Uliopewa na Mungu

Tulipokuwa watoto wadogo, tulikuwa na ndoto za vile tulivyotamani tuwe tukiwa wakubwa. Tulia na fikiria kwa muda kuhusu ndoto zile za utotoni. Je, kuna hata moja ya hizo ndoto iliyotimia katika maisha yako?

Kama vile Mungu alivyokupatia ndoto za thamani za utotoni, anazo ndoto za thamani kwa ajili ya maisha yako leo. Haijalishi mahali ambapo umekuwepo, au kile ambacho umekifanya, haijalishi una umri gani, una jinsia gani, elimu yako au kutokuwa na elimu kwako, mahali unapoishi, au sifa zako, ikiwa unapenda, Mungu atakutumia.

> Kwa watumishi Wake Kristo anatoa "mali Zake"— kitu cha kutumiwa kwa ajili Yake. Anatoa "kwa kila mtu kazi yake." Kila mmoja ana sehemu yake katika mpango wa milele wa mbinguni. Kila mmoja anapaswa kufanya kazi kwa ushirikiano na Kristo kwa ajili ya wokovu wa roho. Kama vile ambavyo kuna mahali katika majumba ya mbinguni kwa ajili yetu kadhalika kuna mahali maalumu duniani palipoteuliwa kwa ajili yetu pa kumfanyia Mungu kazi (Christ's Object Lessons, uk. 326).

Ndiyo, Yesu ana utume maalumu kwa ajili yako kama wewe. Kama vile David Livingstone, mmishenari mashuhuri wa Afrika, alivyowahi kusema wakati fulani, "Ikiwa kushiriki katika utume wa mfalme wa kidunia kunafikiriwa kuwa heshima, kwa nini kushiriki katika utume wa Mfalme wa Mbinguni kunafikiriwa kuwa kafara?"

Omba: Unapoanza kujifunza (au unapojiandaa kufundisha) kanuni ya Kurudi Madhabahuni, mwombe Mungu akupe ujasiri wa kuondoka katika eneo lao la raha kwa njia yoyote kwayo Mungu anakuita kumtumikia. Wakati kila mmoja anazo karama na nguvu fulani, kumbuka, siyo kuwa na sifa

fulani. Ni suala la kuitwa. Anampa sifa kila mtu anayemwita aliye tayari kumtegemea kwa unyenyekevu.

Mwongozo wa Kiongozi wa Kikundi Kidogo

JALI

1. Uliza vikundi vidogo vidogo: "Ni kanuni ipi ya kuishi kama mwanafunzi ina maana zaidi kwako kuliko zingine? Kwa nini?"
2. Hebu tupitie upya kanuni za Kurudi Madhabahuni:
    - Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo!
    - Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana,
        - Sehemu I: Mwombe Mungu akuamshe kila asubuhi uwe na muda usiokuwa na haraka pamoja na Mungu.
        - Sehemu II: Kila asubuhi, iwe kipaumbele chako cha kwanza kutafakari juu ya Yesu alikuwa nani na kile ambacho amekifanya kwa ajili yako. Halafu salimisha vyote ulivyo, vyote ulivyo navyo, na hata mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki kwa Yesu kama Bwana.
        - Sehemu III: Kwa njia ya nguvu ya Yesu anayeishi ndani yako kwa imani, fuata uongozi Wake katika chaguzi zako zote katika siku nzima.
    - Kanuni 3: Mgundue Yesu katika Neno Lake na maombi.
    - Kanuni 4: Omba na pokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu.
    - Kanuni 5: Penda familia yako kwa kudhamiria.
    - Kanuni 6: Wafanye Wengine kuwa Wanafunzi wa Yesu

3. Changamoto ya wiki ya mwisho ilikuwa ni nini? (Chukua wazo ulilolipokea katika mchezo wa "Nifanye Mimi Kuwa Mwanafunzi" na liweke mbele ya Bwana. Liombee. Lifanyie mazoezi. Mwombe Mungu akuoneshe yule ambaye Mungu anapenda umweleze wazo hilo. Omba, na nenda kushiriki wazo hilo na mtu yule.)
4. Shirikiana na mtu fulani. Uliza: "Mungu alikusaidiaje kuishi changamoto kutoka ya wiki iliyopita?" Vipatie vikundi vya watu wawili dakika 2–3 ili wajadiliane. Uliza kundi kubwa lote ikiwa kuna mtu yeyote anapenda kushiriki kile ambacho Mungu alimfanyia katika maisha yake alipoikubali changamoto.

UNGANISHA

1. Wagawanye wote katika vikundi vya watu wawili wawili. Sema: "Fikiria bilionea akikwambia kuwa atakujengea nyumba ya ndoto yako na kuilipia pamoja na ardhi yenye ukubwa wa ekari kumi, mahali popote ulimwenguni. Ungesemaje?"
2. Baada ya vikundi vya watu wawili wawili kusemezana kwa dakika mbili, uliza ikiwa kuna yeyote angependa kushiriki na kundi kubwa.
3. Linaweza kuwa jambo la kufurahisha kuota ndoto kuota aina ya nyumba ambayo tungependa kuishi ndani yake! Unafikiri Mungu ana ndoto gani kwa ajili yako? (Chukua majibu).
4. Tunajua Mungu ana kitu fulani maalumu kilichopangwa kwa ajili yetu mbinguni, lakini tunatumia muda kugundua kile ambacho Mungu amekipanga kwa ajili yetu kumfanyia sasa—kabla hajakuja kutuchukua na kutupeleka mbinguni?

Leo tutachunguza wito wetu wa kipekee na maalumu. Mungu utume kwa ajili maisha yako na ya kwangu. Kuna sababu kwa nini Mungu alituchagua tuishi na kumtumikia sasa.

GUNDUA

Omba: "Mpendwa Mungu Muumbaji, uliziumba mbingu na nchi katika uzuri usiokuwa na kikomo. Ulituumba sisi kama watoto Wako, kila mmoja wetu akiwa wa kipekee na maalumu. Tuamshe tuote ndoto an mipango uliyo nayo kwa ajili ya maisha yetu. Tafadhali, Baba, usituache tupoteze lengo takatifu ambalo ndilo kwalo ulituleta katika ulimwengu huu. Tuoneshe jinsi ya kuishi na kukutumikia sasa—leo! Tuoneshe jinsi ambavyo maisha yetu yanaweza kutumika kwa ajili ya ufalme Wako na kukupatia utukufu na heshima. Katika jina la Yesu, amina."

Ni mambo gani Mungu anayajua juu yako?

Soma: Zaburi 139:1–6, 13–15
Orodhesha mambo ambayo Mungu anayajua juu yako.

Soma: Zaburi 139:16 na Waefeso 2:10
Mambo gani ambayo Mungu ameweka katika maandishi? Ni mambo gani ambayo Mungu aliyapanga kwa ajili yako tangu awali? (Anazo siku zote za maisha yako zikiwa zimewekwa katika maandishi; Anazo kazi njema alizozipanga kwa ajili yako tangu kabla hujazaliwa. Ana utume kwa ajili yako!)

Hebu tuchunguze juu ya Mungu aliyetuumba na jinsi ambavyo alituumba tuwe na jinsi ambavyo tunaweza kumtumikia katika namna yetu wenyewe sasa.

## Gundua Utume Uliopewa na Mungu!

SHUGHULI: Kuchunguza Maswali ya Kujifunzia Mahali pa Kumtumikia Mungu

Tafadhali omba kwa unyenyekevu kabla hujaanza kufanya uchunguzi. Salimisha maisha yako kwa Yesu Kristo. Mwulize Mungu amtume Roho Mtakatifu akuongoze katika mchakato huu.

1. Karama zangu za roho ni zipi?
   Orodhesha karama zote unazofikiri kuwa unazo. Chora duara kuzunguka karama zako 3–5 za juu kabisa.
   - 1 Wakorintho 12:4–11
   - Warumi 12:6–8, 13
   - Waefeso 4:11, 12
   - 1 Petro 4:9–11
   - Kutoka 31:1–5

2. Ni wakati gani nilijisikia sana:
   - Kuwa huru—kuwa kile ambacho Mungu alikuumba ili uwe?
   - Kutiririka—kuwatumikia watu ninaowapenda na kushughulikia mambo ninayoyajali kwa namna ambayo inatumia karama zangu za asili?
   - Kuwa na furaha?
   - Kutumiwa na Mungu?
   - Kupata mrejesho chanya kutoka kwa watu walioitikia huduma yangu kwa kuja kwa Mungu?

Kwa kifupi shiriki mara tatu katika maisha yako wakati mambo hayo matano yalipokuwepo kwa ajili yako.

3. Ni nani ningependa kumsaidia?
   Orodhesha aina /makundi ya watu una moyo wa kuwasaidia. Zungushia duara mambo 3-5 ya juu kabisa.

4. Ni mambo gani ninayajali?
   Orodhesha mambo ambayo hupuuzwa katika ulimwengu wako yanayokufanya uwe na hasira. Au orodhesha mambo ambayo unatamani kuyashughulikia.

5. Unaona nini ndani yangu?
   Tuma majibu yako kwa maswali manne ya mwisho kwa watu watano walio na vigezo vifuatavyo:
   - Wanakujua vizuri.
   - Wanakujali.
   - Wanatembea na Mungu.
   - Wana utambuzi.
   - Watatumia siku tatu wakiomba na kutafakari juu ya majibu yako na utajibu swali hili: "Ni katika njia zipi mahsusi unafikiri ninaweza kumtumikia Mungu kwa karama zangu, kwa kuzingatia maslahi ya watu na masuala ninayoyajali?"

   Ombea mambo ambayo watu hawa watano wanakupatia. Tafuta hekima ya Mungu ya Yakobo 1:5–8. Chukua hatua za imani za kumtumikia Mungu katika namna ambayo Mungu anakuita kuifuata!

## Ishi Ombi la Bwana wa Mavuno

Tafakari juu ya Mathayo 9:35–38:

- Aya 35 – Yesu alifundisha, alitangaza injili, na aliponya. Mambo haya matatu yalikwenda pamoja!
- Aya 36 – Yesu aliwaona watu na aliona huruma kwa ajili ya makutano.

- Aya 37 – Yesu aliona mavuno yakiwa mengi lakini wavunaji wakiwa wachache.
- Aya 38 – Yesu anawaambia wanafunzi Wake wamwombe Bwana wa mavuno a- ekballo—maana yake, avurumishe watenda kazi katika mavuno Yake.

Mathayo 10:16 – Yesu hatuiti ili tuombe tu ili awatume wengine katika mavuno; Anatuambia sisi twende wenyewe! Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu atupatie sisi vipawa vyema vyote  na hutuagiza tusiwe na woga na tuwe waaminifu katika utume Wake!

Vurumisha katika Mavuno – Shughuli ya Kufungia

- Shiriki: Tulijifunza kuwa Yesu anataka kutuvurumisha twende katika Mavuno Yake. Anataka aturushe wewe na mimi hadi katika utume ambao ameuota kwa ajili yetu.
- Mafundisho: Mwelekeze kila mmoja achukue kipande cha karatasi na aandike juu yake utume unaokuondoa katika ukanda wako wa raha ambao Mungu anawagusa kuutekeleza. Inawezekana ikawa kumshuhudia jirani sehemu fulani mtaani kwako, kufanya urafiki na mnyanyasaji shuleni, au jambo fulani linalohitaji uamuzi mgumu zaidi kama vile kuacha kazi na kwenda kuishi sehemu ya mbali kwa ajili ya kufanya wanafunzi.
- Baada ya kila mmoja kuwa ameandika kitu fulani kwenye karatasi, waalike wakusanyike pamoja, waunde mduara mkubwa na kila mtu akiwa ametazama nje ya mduara. Waelekeze wachukue karatasi ambazo ndiyo tu wameziandika wazikunje na kuzivingirisha ili kupata mpira mgumu. Mwalike kila mmoja kuvurumisha au kurusha mpira wa karatasi kwenda mbali ya duara kwa kadiri iwezekanavyo.
- Uliza: "Je, mtu yeyote anaweza kushiriki utume wake wa nje ya kanda ya raha ambayo ameiandika na kuivurumisha katika mavuno?"
- Baada ya kupata majibu machache, uliza mtu yeyote mmoja anayependa kujitokeza na kuondoka katika eneo lake la raha, na kwenda mahali mahali ambapo kipande cha cha karatasi kiliangukia, na tumia dakika tano kujisalimisha kwa Yesu kwa siri, akimwomba Yesu

amvurumishe na kumwigiza katika utume ambao Yesu ameota kwa ajili yake kabla hajazaliwa!

- Baada ya dakika tano, imba korasi fupi ya kuwaita watu wote katika kikundi warudi na kukusanyika pamoja. Pigeni magoti na kuomba pamoja.

Omba: "Baba mpendwa wa mbinguni, asante kwa kutuita ili tumfuate Mwana Wako kama wanafunzi Wake! Tunajisalimisha kwa Yesu kama Bwana na tunaomba kuwa atuvurumishe na kutuingiza katika mavuno Yake mahali popote anapotaka kututuma. Tupatie ujasiri wa kutii mara tu anapotuita kwa ajili ya utume Wake wa injili. Katika jina la Yesu, amina."

CHANGAMOTO YA KURUDI MADHABAHUNI – Kanuni 7
Jibu maswali yote ya "Wapi pa Kumtumikia Mungu?," omba mrejesho kutoka marafiki na wanafamilia, ombea matokeo ya kufuata uongozi wa Mungu, na kutumika mahali anapokuongoza!

Kwa kuhitimisha, kumbuka hili:

> Hakuna ukomo wa manufaa ya yule ambaye, kwa kuweka ubinafsi kando, anaacha nafasi kwa ajili ya utendaji kazi wa Roho Mtakatifu juu ya moyo wake, na anaishi maisha yaliyowekwa wakfu kikamilifu kwa Mungu. Ikiwa watu watavumilia nidhamu ya lazima, bila kulalamika au kuzimia njiani, Mungu atawafundisha saa baada ya saa, na siku kwa siku. Anatamani kufunua neema Yake. Ikiwa watu Wake wataondoa vipingamizi, Mungu atamimina maji ya wokovu katika vijito vya wingi kupitia katika mifereji ya kibinadamu. Ikiwa watu wanaoishi maisha ya kawaida wangetiwa moyo kufanya mambo yote mema ambayo wana uwezo wa kuyafanya, ikiwa mikono inayozuia isingewekwa juu yao kudhoofisha juhudi yao, kungekuwa na watendakazi mia moja kwa ajili ya Kristo mahali ambapo sasa kuna mtenda kazi mmoja (The Desire of Ages, uk. 250).

Na chochote mnachokifanya, kiwe sahili! Kuhubiri kuwe kudogo, kufundisha kwingi, na muda mwingi utumiwe katika Neno.

> Inapasa kuhubiri kuwe kudogo, na kufundisha kuwe kwingi … Tunapokaribia mwisho, nimeona kuwa katika mikutano hii kutakuwa na kuhubiri kudogo, na kujifunza Biblia kwingi. Kutakuwa na vikundi vidogo vidogo katika viwanja, na Biblia mikononi mwao, na watu mbalimbali wakiongoza katika maongezi ya mafundisho huru, ya nje, ya Maandiko. Hii ndiyo ilikuwa mbinu ambayo Yesu aliitumia kufundisha wanafunzi Wake (Gospel Workers, uk. 407).

"Si kwa uwezo, wala si kwa nguvu, bali ni kwa
roho yangu, asema Bwana wa majeshi."
(Zek. 4:6)

Hatua Inayofuata …

# Vipi Ikiwa Utaishi Kama Mwanafunzi wa Yesu?

Uliza kikundi:

- "Ikiwa ungeishi kama mwanafunzi wa Yesu (kila siku, matokeo yake yangekuwaje?" (Subiri majibu.)
- "Mungu angependa kufanya nini nasi wakati mwingine kama kikundi?"

Ombeni pamoja katika makundi ya watu wawili wawili na halafu ombeni ombi moja la pamoja, mkimwuliza Mungu kile ambacho angependa kifanywe na kikundi. Baada ya kuomba, waulize watu waseme. Panga mipango kulingana na kile ambacho Mungu amekifunua kwa kikundi.

## Mungu anatutaka tufanye wanafunzi:

- Akina Nuhu, wanaojenga kitu ambacho hakijawahi kujengwa kabla.
- Akina Ibrahimu, wanaoondoka katika nchi zao na kwenda katika nchi ambazo Mungu atawaonesha.
- Akina Yusufu, wanaokataa kushusha viwango vyao na ambao Mungu atawapa dhamana ya ndoto ya kuongoza mataifa.
- Akina Musa, ambao Mungu atawapa zana mpya katika miaka yao ya uzeeni kuongoza watu Wake kwenda mahali wanapaswa kwenda.
- Akina Bezaleli, watakaosanifu na kujenga kile ambacho mwanadamu hawezi kufikiria.
- Akina Yoshua, wanaodiriki kuomba maombi ya kusimamisha jua.
- Akina Debora, watakaoongoza watu wa Mungu kwa hekima itokayo juu mbinguni.

- Akina Samueli, ambao katika utoto wao wataisikia sauti ya Mungu, wamjue, na kuwaita watu Wake kuwa waaminifu.

- Akina Ruthu, wanaokataa kuruhusu misiba yao kuamua hatima ya maisha yao, wanaompenda yule ambaye Mungu amewapa, na wanaoacha nyuma urithi wa imani.

- Akina Ayubu, ambao ni wafanyabiashara wakubwa, watakaodumu kuwa waaminifu kwa Mungu wakati wa uwingi wa mali na wakati wa majanga na misiba, na watakaowatunza wajane na yatima.

- Akina Eliya, watakao wakabilia watu waovu wenye vyeo vya juu, kuyaita mataifa kufanya uamsho, kuita moto kutoka mbinguni, kuwainua akina Elisha, na kuvuka mito ya Yordani.

- Akina Elisha, watakaookota joho katika ujana wao, kupiga maji ya Yordani, kuvuka Yordani, na kuwaongoza watu wenye nguvu kumjua Mungu.

- Akina Daudi, watakaowakabili na kuwaua majitu na kuwaongoza watu wenye nguvu.

- Akina Isakari, wanaojua nyakati na kile ambacho Israeli wanapswa kukifanya.

- Akina Yona, wanaoacha kumkimbia Mungu ili watumwe kuiita miji yote isiyomcha Mungu itubu na kumrudia Mungu.

- Akina Yeremia, wanaotabiri ukweli hata wakati watu hawataki kuusikia.

- Akina Danieli, ambao hawatanunuliwa au kuuzwa, walio watiifu kwa Mungu kwa gharama yoyote, wanaosimama kwa ajili ya Mungu dhidi makutano ya watu, wanaoongoza mataifa na kuwashauri wakuu wa nchi, kuwafanya waovu wenye vyeo vya juu kuwa wanafunzi na kuwafanya watembee pamoja na Mungu.

- Akina Esta, watakaosimama mbele ya watu wakuu wa dunia na kuhatarisha maisha yao ili kusaidia kuwaokoa watu wa Mungu.

- Akina Mariamu, ambao katika maisha yao ya ujana wanakuwa jasiri na kukabiliana na dhihaka kwa kusema, “Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana; na iwe kwangu kama ulivyosema.”

- Akina Mariamu Magdalena, wanaobadilishwa kutoka wanawake wa usiku na kuwa binti wa Nuru, wanaosimama kwa nguvu ya Mungu peke yake na wanaponywa kwa uwepo wa ufufuko Wake.

- Akina Andrea, ambao kimya kimya bila kuchoka huleta watafutaji kwa Yesu.

- Akina Petro, wanaoacha mitumbwi yao na kujiunga na Yesu ili kutembea juu ya maji.

- Wajane, wanaotoa vyote walivyo navyo kwa Yesu.

- Akina Lydia, watakaokuwa wajasiriamali wenye moyo wa kuhudumia na nyumba kwa ajili ya ukarimu.

- Akina Barnaba, ambao ni wana wa faraja na wanaowalea watu wenye nguvu kwa ajili ya Kristo.

- Akina Luka, watakaokuwa waganga wamishonari will, wakichanganya injili na dawa.

- Akina Yusufu wa Arimathaya, watu wenye mali wanaohatarisha vyote kwa ajili ya Kristo na wanaotumia mvuto wao kwa ajili ya ufalme wa Mungu.

- Akina Suzana, ambao ni ushuhuda unaotembea wa uponyaji na ukombozi, wanaomfuata Yesu mahali kote anakokwenda na wanategemeza huduma kwa fedha yao.

- Akina Paulo, watakaoteseka na kutoa kafara ya raha yao na usalama wao ili kuchukua Injili kwa wale ambao hawajasikia chochote kuhusu Yesu, ambao watahatarisha vyote ili wawe mitume katika maeneo ya watu wasiokuwa wakarimu, wanaoandikwa kinachopaswa kuandikwa na kutangaza uhuru kwa gharama ya maisha yao wenyewe kwa wale wanaolia wakiwa gizani.

Kiambatanisho 1

# Usiku wa Maombi

Mfano wa Yesu

"Ikawa siku zile aliondoka akaenda mlimani ili kuomba, akakesha usiku kucha katika kumwomba Mungu. Hata kulipokuwa mchana aliwaita wanafunzi wake; akachagua kumi na wawili miongoni mwao, ambao aliwaita Mitume; Simoni, aliyemwita jina la pili Petro, na Andrea nduguye, na Yakobo na Yohana, na Filipo na Bartolomayo, na Mathayo na Tomaso, na Yakobo wa Alfayo, na Simoni aitwaye Zelote, na Yuda wa Yakobo, na Yuda Iskariote, ndiye aliyekuwa msaliti" (Luka 6:12–16).

"Yeye asemaye ya kuwa anakaa ndani yake, imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda" (1 Yohana 2:6).

Changamoto

Yesu alitumia usiku wa maombi kabla ya hajachagua wanafunzi Wake kumi na wawili. Tumia usiku wa maombi kumwabudu Mungu na kumwomba na kupokea maelekezo kuhusiana na maswali mawili:

1. Mungu, ni nani unayetaka nimfanye kuwa mwanafunzi wa Kristo wakati huu?
2. Mungu, ni kwa jinsi gani unanitaka niendeshe maisha / huduma yangu wakati huu?

Vidokezo kwa ajili ya Usiku wa Maombi

- Njoo katika uwepo wa Mungu ukiwa na shukurani. Furahia kupitia upya njia zote ambazo Mungu amekuwa akifanya kazi katika maisha yako na mshukuru kwa ajili ya baraka hizi (Zaburi 100:4).
- Msifu Mungu kwa vile alivyo! Ni kwa jinsi gani Mungu amejifunua kwako? Mpe utukufu kwa ajili ya tabia Yake, nguvu Yake, na ufalme Wake (Zaburi 100:4).
- Jisalimishe kikamilifu (Mathayo 28:18 na Wafilipi 2:5–11) kwa Yesu kama kwa Bwana kuhusiana na mambo yafuatayo:

    - Vyote ulivyo kama mtu—utambulisho wako, mafanikio yako, na kushindwa kwako
    - Vyote ulivyo navyo—muda wako, talanta zako, mzali zako, na mvuto wako
    - Mtazamo wako na vifaa vyako vya kielektroniki
- Ungama dhambi zako na dai msamaha wa Mungu (Zaburi 51:10–12 na 1 Yohana 1:9).
- Mwalike Mungu atafute dhambi yoyote au mifumo yoyote ya dhambi ambayo unaiungama daima lakini hauachani nayo (Matendo 2:38, 39). Tubu dhambi hizo. Ikiwa hujisikii kutubu, omba Ezekieli 36:25–27, ukidai ahadi hizi kama zako.
- Mwombe Mungu akupe:
    - Ubatizo wa Roho Mtakatifu (Luka 11:11–13 na Matendo 1:4, 5).
    - Hekima ya kujua mtu ambaye Mungu anataka umfanye kuwa mwanafunzi to sasa (Isaya 30:21).
    - Omba: "Mungu, ni nani unayetaka nimfanye kuwa mwanafunzi ili awe mfanya wanafunzi katika wakati huu wa mwisho?" (Yakobo 1:5–8).
    - Uongozi wa jinsi Mungu anavyotaka uendeshe maisha/huduma yako sasa (Mithali 3:5, 6).
- Ngoja kwa matarajio (Yeremia 33:3; Zaburi 25:4, 5; Zaburi 46:10).
- Pima mahitimisho yako kwa Neno la Mungu (Isaya 8:20). Omba: "Bwana, kuna jambo lolote katika Neno Lako kinachopingana au kuchothibitisha mahitimisho yangu?"
- Shukuru Mungu kwa kutumia usiku wa maombi pamoja nawe (1 Thes. 5:18).

<u>Viashiria</u>

Uliza marafiki na/au wanafamilia kuomba kwa ajili yako wakati huu.

Yesu alitumia usiku kucha katika maombi. Hatujui yalikuwa masaa mangapi; ilikuwa tu "usiku." Usikazie kuhusu "usiku" wako ni mrefu au mfupi kiasi gani. Wewe tu mpe Mungu muda na mruhusu Roho Mtakatifu akuongeze wakati wa kuhitimisha. Mungu anajua ukomo wako binafsi kuliko wewe unavyojua. Muhtasari huu ni zana tu. Salimisha zana hii kwa uongozi wa Roho Mtakatifu aibadilishe kulingana na jinsi anavyotaka Mwenyewe.

Kiambatanisho 2

# Jinsi ya Kutoa Ushuhuda Wako

Chunguza ushuhuda wa mtume Paulo kwa kusoma Matendo 21:39–22:21, Wafilipi 4:10-13, na 1 Petro 3:15-17.

Njia rahisi ya kufikiria juu ya ushuhuda wako binafsi (kisa chako na cha Yesu Kristo) kuuandaa katika sehemu tatu:

1. Kabla ya Kristo: Eleza kwa kifupi jinsi maisha yako yalivyokuwa kabla ya kusalimisha maisha yako kwa Yesu Kristo kama Mwokozi na Bwana wako. Eleza kilichokuwa kinakosekana katika maisha yako. Usiyafanye maisha yako ya dhambi yaonekana kuwa ya kuvutia.
2. Jinsi ulivyokutana na Kristo: Eleza jinsi Yesu alivyoingilia kati katika maisha yako. Ni kwa jinsi alikufanya umsikilize? Ni kwa jinsi gani alikuita ukamwendea? Jumuisha aya ya Biblia au kifungu cha maneno ya Biblia ikiwezekana.
3. Jinsi Yesu anavyoendelea kukubadilisha: Eleza tofauti ambayo Yesu Kristo ameileta katika maisha yako. Kwa nini unampenda na kumtumikia? Amefanya nini kwa ajili yako? Hadhira yako inahitaji kuona kitu kipya katika safari yako ya kiroho —eleza tofauti anayoileta katika uzoefu wako wa kila siku sasa! Ni jambo gani ulilonalo katika utembeaji wako na Yesu ambalo ungependa wengine wanahitaji wawe nalo? Hii inapaswa kuwa sehemu tamu zaidi kuliko sehemu zote za ushuhuda wako.

Andika ushuhuda wako. Hakikisha inajumuisha angalau Andiko 1 au Maandiko 2. Unaweza kuandaa maelezo ya aina tatu ya ushuhuda huo huo:

- Maelezo mafupi ya dakika moja ya kwenda lifti—kwa maneno mengine, ushuhuda unaoweza kuutoa katika dakika moja ukiwa katika lifti.
- Maelezo ya muhtasari wa dakika 5—ukitoa vipengele vya thamani na mawazo maalumu machache.
- Maelezo ya dakika 10 hadi15, yenye maelezo ya kina na shuhuda za uingiliaji kati wa Mungu na uongozi Wake.

Baada ya kumaliza kuandika ushuhuda wako, ujisikie kuwa na furaha kuwaeleza wengine. Ikiwa ulikuwa hujawahi

kueleza kabla, fanya mazoezi kwa kumsimulia rafiki, mlezi wako, au mwanafamilia.

Kumbuka, uwe mkweli na halisi na mwenye furaha. Uko safarini pamoja na Yesu. Maisha yako siyo tu ya kwako pekee yako au ya kujitafutia utukufu wako mwenyewe. Ni suala la kumletea Mungu utukufu. (Tazama Zaburi 115:1.)

"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu" (1 Petro 2:9).

"Kwa sababu hiyo ninyi ni mashahidi wangu," asema Bwana, "nami ni Mungu" (Isa. 43:12).

Kiambatanisho 3

# Mawazo Kuhusu Kupanga Ibada za Familia

- Hakikisha Muda wa ibada uwe mfupi. Kwa kadiri mtoto a navyokuwa mdogo zaidi, ndivyo na ibada inapaswa kuwa fupi zaidi. Dakika tatu mpaka tano zinazomwunganisha mtoto mdogo na Mungu ni bora zaidi kuliko dakika 15–20 zinazomwacha mtoto akiwa amechoshwa na akiwa ameondoa akili yake. Urefu wa ibada unaweza kuongezwa kwa kadiri umri wa mtoto unavyoongezeka.

- Fokasi muda wako kwa Mungu. Usitumie muda kuwakosoa wanafamilia; badala yake, sherehekea vile Mungu alivyo na kile ambacho anatamani kufanya katika na kupitia familia!

- Tumia muda pamoja kwa kujadiliana kuliko kusoma au kutoa muhadhara peke yake.

- Fikiria njia zifuatazo za kufanya ibada ya Mungu iwe ya majadiliano:
    - Shiriki kile ambacho Mungu alikifanya wakati wa mchana na umshukuru.
    - Msifu Mungu kwa ajili ya kile unanchokipenda kumhusu mungu.
    - Ikiwa familia yako inapenda kuimba au kucheza ala za muziki, msifu Mungu kwa njia ya nyimbo.
    - Mwombe Mungu amtume Roho Mtakatifu abariki kile mnachokisoma katika Biblia.
    - Buni shughuli, rahisi, inayochekesha inayounganisha akili na mioyo ya wanafamilia na wazo kuu mtakalolichunguza katika Bibla.
    - Chunguza kisa cha Biblia ukiwa na fokasi ya kumgundua Yesu. Uliza:
        - Kisa hiki kinatuonesha nini kuhusu Yesu alivyo?
        - Mungu anatuita tufanye nini leo katika somo la kisha hiki?

- Mwombeni Mungu pamoja awasaidie kuuishi ukweli kuhusu Yesu.

## Maswali ya Kujiuliza Unapotayarisha Ibada ya Familia

1. "Yesu amekuwa akifanya nini moyoni mwangu mwenyewe?" Shirikisha kutoka kwenye uzoefu wako wa sasa wa kuishi na Yesu.
2. "Neno la Mungu linagusaje moyo wangu mwenyewe kwa sasa?" Shirikisha kitu kipya na cha hivi karibuni ambacho umegundua katika Neno la Mungu.
3. "Mahitaji ya sasa ya wanafamilia wangu ni yapi? Wanapitia nini maishani mwao?"
4. "Ni kifungu gani cha Maandiko kinachozungumza kwa ufanisi zaidi kwa mahitaji ya sasa ya moyoni ya familia yangu?" Huu sio wakati wa kuhubiri, lakini ni fursa ya kushiriki uponyaji na tumaini.
5. "Ni shughuli gani ya kufurahisha ambayo ingemuunganisha kila mwanafamilia na Maandiko ambayo nitashiriki kwenye ibada?" (Angalia mifano ya ubunifu kwenye kurasa zifuatazo.)
6. "Ni maswali gani ninapaswa kuuliza ambayo yanaweza kusaidia familia yangu kuchunguza Neno na kumgundua Yesu?"
7. "Ninawezaje kuhimiza familia yangu kutumia kile walichojifunza katika maisha yao ya kila siku?"

## Mfano wa Mtiririko wa Ibada shirikishi ya Familia

1. Shughuli ya Unganisha
    - Ufupisho
    - Maombi
2. Chunguza Neno
3. Litumie neno
    - Nyimbo zinazoendana na mada iliyochaguliwa zinaweza kuongezwa
    - Ombi la mwisho

## Mifano ya Ibada ya Kiubunifu

Mawazo ya ibada yafuatayo yamekusudiwa kukupatia tu mahali pa kuanzia. Badilisha mawazo yafae kwa ajili ya kundi la umri. Mwombe Roho Mtakatifu akuongoze na kukuonesha

jinsi ya kuunganisha moyo na moyo na mwenzi wako na watoto wako.

Kwa mbaraka wa Bwana, ibada za kila siku za familia zinaweza kuwa wakati ambao kila mmoja katika familia anatamani ufike haraka.

<u>Jenga Imani</u>

Maandiko: Mithali 3:5, 6
Neno Kuu: Imani
Shughuli ya Kuunganisha: Anguko la Imani
Mwombe mwanafamilia mmoja asimame mikono yake ikiwa kando yake. Weka wanafamilia wawili nyuma yake mikono yao ikiwa imefungwa pamoja, tayari kumdaka. Mwalike yule mtu aangukie nyuma bila kukunja magoti yake.
Mjadala: Jadilini maana ya kuaminiana na kinachomaanisha kumwamini Mungu.
Omba: Mwombe Mungu akusaidie kumgundua Yesu katika njia mpya katika kisa cha Biblia.
Gundua: Soma Mathayo 14:22–33 na Mithali 3:5, 6.

- Kisa hiki kinatuonesha nini kumhusu Yesu?
- Ni jambo tunahitaji kumwamini Yesu kikamilifu leo?

Omba: Ombeni pamoja ili Mungu akusaidie umwamini Yesu kikamilifu leo.

<u>Kulifuata Neno</u>

Maandiko: Zaburi 119:105
Neno Kuu: Neno la Mungu
Shughuli ya Kuunganisha: Ifuate Nuru
Chagua mtu mmoja ashike tochi. Jipangeni katika mstari nyuma ya mtu yule mwenye tochi. Zimeni ta azote katika nyumba. Washa tochi na mmfuate kiongozi aliyeshika mwanga.
Mjadala: Jadilini jinsi Neno la Mungu linavyofanana na mwanga katika giza.

Omba: Mwombeni Mungu awasaidie kumgundua Yesu katika njia mpya katika kisa cha Biblia.

Chunguza: Soma Zaburi 119:105 na Matendo 8:25–40.

- Kisa hiki kinatuonesha nini kumhusu Yesu?
- Ni kwa jinsi gani tutafanyia mazoezi ya kufuata Neno la Mungu leo kama mwanga wa njia yetu?

Omba: Mwombeni Mungu pamoa awasaidie kulifuata Neno kama mwanga katika.

<u>Kumwona Yesu</u>

Maandiko: Yohana 15:5

Neno Kuu: Uzima wa Milele

Shughuli ya Kuunganisha 1: Kumwona Yesu katika Maisha ya Kila Siku

Kila mtu apewe zamu ya kueleza jinsi alivyomwona Yesu kazini katika safari yenu—katika nyakati nzuri na za mambo magumu yaliyotokea.

Shughuli ya Kuunganisha 2: Kumwona Yesu Ndani ya Kila Mmoja. Tumia muda kujaza nafasi iliyo wazi, "Nilimwona Yesu ndani ya __________ (jina la mwanafamilia) leo ana/au juma hili __________(jaza katika nafasi)."

Mjadala: Elezea jinsi ulivyomwona Yesu ndani ya kila mmojawenu kupitia shughuli za kila siku. Jambo hili huwezesha wanafamilia kukubali na kukubaliwa katika uhalisia wa Kristo anayeishi ndani yao na kupitia kwao kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Omba: Omba kuwa unaweza kumgundua Yesu katika njia mpya katika Neno Lake.

Gundua: Soma Yohana 15:5 tena na Wagalatia 5:22, 23.

- Maandiko haya yanatufundisha nini kumhusu Yeus anayeishi ndani yetu?
- Ikiwa Yesu anaishi ndani yetu, ni aina gani ya matunda (mitazamo/matendo) yataonekana ndani yetu?

Omba: Ombeni pamoja ili Yesu aishi ndani yenu na kufanya makao Yake pamoja nanyi. Ombeni kuwa tunda Lake lionekane ndani ya maisha yenu.

<u>Gudulia la "Maombi Yaliyojibiwa"</u>

Andaa: Pata magudulia mawili ya glasi. Bandika lebo kwenye gudulia moja "Mambo ya Kuombea" na jingine "Maombi Yaliyojibiwa." Pata kadi au karasi zenye ukubwa wa inchi 3x5.

Andika: Kama familia, andika mambo yako ya kuombea kwenye kadi tofauti za rangi za nchi 3x5. Waulize watoto

wako wakupatie mambo yao ya kuombea. Tafuta aya ya Biblia unayoweza kuandika nyuma ya kila kadi. Wafundishe kwanini tunadai Neno la Mungu kwa ajili ya maombi yetu (tazama Isa. 55:11). Weka maombi yenu yote katika gudulia lililoandikwa "Mambo ya Kuombea."
Omba: Katika kila ibada, vuta gudulia la "Mambo ya Kuombea" na liweke katikati ya duara la familia wakati mnaomba. Ikiwa una muda, vuta na kutoa nje baadhi ya maombi na kuyaombea. Ombebi maombi mafupi, katika mtindo wa maongezi wakati mwanafamilia tofauti akishika zamu yake kuchangia katika maombi ya familia nzima.
Sherehekea: Wakati wowote ombi linapojibiwa, uwe na mpatie mtoto afurahie kuhamisha ombi lile na kuliweka katika gudulia la "Maombi Yaliyojibiwa." Halafu sherehekea kwa kumsifu Mungu. Watoto wa umri wote hupenda kuangalia gudulia la maombi yaliyojibiwa likijaa, na jambo hilo hujenga imani zao.

Zawadi Nzuri Kabisa!*
Andaa: Tambua angalau karama mbili za kiroho unazodhani Mungu amewapa kila mmoja wa watoto wako. Tafuta kitu cha kufananisha na karama hizi na kivingirishe katika karatasi za kufungia zawadi na kukifunga kwa riboni za kufungia zawadi.
Soma: Soma 1 Wakorintho 12:1–11 na wape watoto wako zawadi zao, ukithibitisha ushahidi uliouona unaoonesha kuwa Mungu ameweka karama hizi juu yao. Wape watoto wako nafasi ya kufikiri juu ya jinsi watakavyofurahia karama hizi na kuzitumia kutangaza Habari Njema juu ya Yesu na katika huduma kwa wengine.
Omba: Waweke wakfu watoto wako na karama zao kwa Mungu upya.

Katika Utume*
Soma: Mathayo 28:19, 20. Mnajionaje wenyewe katika picha hii? Andika tamko la utume kwa ajili ya familia yako.

Omba: Ombeni pamoja kwa ajili ya kauli ya utume wa familia.
Panga: Panga mpango wa ninyi kama familia mnavyoweza kuanza kuishi tamko lenu la utume kiutendaji.

Shinda Milima*
Soma: Isaya 40:28–31
Siri ya kupata nguvu mpya ni nini? Nini maana ya kumngoja Bwana?
Jadili: Ni jambo gani linalokufanya ujisikie kuwa na nguvu, mathalani ungeweza kupanda Mlima? Shiriki na familia yako wakati Mungu alipokupatia nguvu mpya. Waombe wanafamilia wa familia yako waeleze mmoja baada ya mwingine njia za kiutendaji amazo kwazo wanaweza kuwa “upepo chini ya mbawa za mwenzake” wiki hii.
Omba: Ombea aya hii ya Biblia kwa ajili ya maisha yenu kama familia.

Farijika*
Uliza: Mwulize kila mwanafamilia kuleta katika ibada ya familia kitu fulani kinachowafariji wanapokuwa wamechoka, wanapokuwa wanaumwa, au wanapokuwa wana wasiwasi. Pengine ni blanketi nzuri, kinyaji cha moto, mwanasesere laini, losheni yenye harufu nzuri, n.k.
Soma: Isaya 40:1, 2
Jadili: Zungumzeni pamoja kuhusu faraja inayotokana na kujua kuwa Mungu ameupatanisha ulimwengu wote na nafsi Yake katika Yesu Kristo na kuwa wewe ni sehemu ya ulimwengu huo uliorudishwa katika familia ya Mungu. Sherehekea uamuzi wenu wa kupokea zawadi hii kutoka kwa Mungu kwa kusimama katika duara na kunyosha ngumi zenu zilizofungwa imara, halafu kukunjua vidole kupokea wokovu wenu katika Yesu.

ABC za Sifa na Ibada*
Unganisha: Eleza kwa nini uliwapa watoto wako majina uliyowapa na fafanua kwa nini majina yao ni maalumu.
Soma: Wafilipi 2:9–11
Chunguza: Fikirieni juu ya majina yote ya Kristo mnayoweza kuyapata katika Biblia. Jaribuni muone kama inawezekana kupata angalau jina moja kwa kila herufi ya alfabeti.

Jadili: Jadilini juu ya majina tofauti mliyoyapata na jinsi yalivyo na maana katika maisha yenu.
Sifu: Tumieni muda wa kutosha kupitia ABC za sifa, mkimsifu Mungu kwa kila moja ya majina mliyoyapata. Kwa nyongeza,

gundueni ni mambo mangapi mnaweza kuyafikiria ya kumsifu Mungu kwa kutumia kila moja ya herufi za alfabeti. Msihamie kwa herufi inayofuata mpaka mtu yeyote miongoni mwenu hawezi kufikiri juu ya wazo zaidi ambalo kwalo angemshukuru Mungu.

*Tunaishukuru Idara ya Huduma za Familia za Kiadventista kwa ajili ya mawazo haya ya ibada. Viungo kwa ajili ya mafundisho zaidi ya familia, vijana, na watoto vimejumuishwa mwishoni mwa kijitabu hiki.

## Vidokezo vya Kurudi Madhabahuni kwa Ajili ya Wanandoa

Kaya na ndoa yako vinaweza kuwa mbingu ndogo duniani!

- Jitoe upya kumtafuta Mungu wewe binafsi na pamoja na wengine katika familia katika ibada kila siku.
- Iwe kipaubele chako kuomba pamoja kila siku, mkimwomba Roho Mtakatifu kudumisha mioyo yenu katika umoja na afanye kazi kupitia ndoa yenu.
- Uwe mnyenyekevu! Wakati makosa yanapotokea, omba msamaha haraka. Tumeambiwa, "Ikiwa kiburi na ubinafsi vingewekwa kando, dakika tano zingeondoa matatizo yaliyo mengi" (Early Writings, uk. 119).
- Dumisha ibada ya wanandoa kuwa fupi lakini yenye maana na inayogusa mahitaji.
- Chagua aya moja au shiriki kifungu cha maneno kifupi cha kuchunguza katika Maandiko: Mtafute Yesu, msifu kwa vile alivyo, na tafuta matumizi halisi katika maisha ya kila siku. Omba na tumia!
- Wakati muda unaporuhusu, jifuneni pamoja Biblia kwa kina zaidi, mkijifunza mhusika wa Biblia, kitabu cha Biblia, au mada mahsusi. Chunguzeni Neno pamoja na mmruhusu Roho Mtakatifu awaongoze. (Tazama Kiambatanisho 7 kwa ajili ya Funguo za Kupata Uzoefu wa Neno la Mungu.)

> "Chanzo cha migawanyiko na mitafaruku katika familia na katika kanisa kujitenga na Kristo. Kuja karibu na Kristo ni kuja karibu na mwenzako. Siri ya umoja wa

kweli katika kanisa na katika familia siyo diplomasia, siyo usimamizi, siyo juhudi isiyokuwa ya kibinadamu ya kushinda matatizo—ingawa yatakuwepo mengi ya kufanya kama haya—bali ni muungano na Kristo. Kwa kadiri tunavyokuja karibu na Kristo, ndivyo tutakavyokuja karibu kila mmoja na mwenzake" (The Adventist Home, uk. 179).

"Aina ya mbingu iliyo tamu zaidi kuliko zote ni kaya ambayo Roho wa Bwana anatawala" (The Adventist Home, uk. 15).

Kiambatanisho 4

# Kutafuta Utume Wako Uliopewa na Mungu

(na jinsi ya kuyajua mapenzi ya Mungu kwa ajili ya maisha yako)

## Maswali Matano ya Kuuliza

Nehemia 1 na 2

1. Soma Nehemia 1:1–4. Nehemia alihuzunishwa na kuta za Yerusalmu zilizobomoka. Utume unaotolewa na Mungu hushughulikia kitu ambacho Mungu huturuhusu kukiona ambacho kimevunjika katika ulimwengu wetu. Kitu gani amacho kimevunjika karibu yako ambacho kinaufanya moyo wako uhuzunike? Mwombe na mwulize Mungu akusaidie kutambua mambo yaliyo katika ulimwengu ambayo amekupatia macho ya kuyaona. Uwe mahsusi kwa kadiri iwezekanavyo. Punguza majibu yako hadi ubaki na suala moja ambalo Mungu amekupatia shauku kubwa zaidi kuliko mambo mengine ili uyashughulikie. Elezea suala hili, jambo hili lililobomoka, katika sentensi moja.
2. Soma Nehemia 1:4–10. Nehemia alitenga siku za kufunga na kuomba juu ya kuta zilizobomoka. Umefanya yafuatayo kama majibu kwa kile ambacho Mungu amekuonesha kuwa kimevunjika:
    - Umemsifu Mungu kwa sababu ya jinsi vile alivyo?
    - Umeungama dhambi zako?
    - Umeziungama dhambi hizi? (Kugeuka na kuziacha dhambi hizi kwa nguvu ya Yesu Kristo.)
    - Umefunga? (Kwa nini ufunge? Kujinyenyekeza mbele ya Mungu na kusafisha akili yako ili uweze kuitambua uongozi waa Mungu.)
    - Umezidai ahadi za Mungu? (Tambua ahadi za Mungu katika Neno Lake ambazo zinapatana na ndoto ya Mungu kwa ajili yako. Chagua kuamini ahadi hizi. Mwombe Mungu kwa imani atimize ahadi hizi kwa ajili ua utukufu Wake.)
3. Soma Nehemia 1:11. Nehemia aliomba upendeleo kwa mfalme. Aikuwa tayari kwa ajili ya kazi ya Kimungu. Wakati mfalme alipomwuliza swali, Nehemia alikuwa na

uchaguzi: kujibu kwa imani au kwa hofu. Kazi za Kimungu huanzishwa na Roho Mtakatifu kupitia kwetu au kwa watu mwingine. Roho Mtakatifu anaweza kukueleza kuchukua hatua ya kwanza au anaweza kumwambia yule mtu mwingine kuanza mazungumzo. Umemwomba Mungu kwa ajili ya maongezi ya Kimungu na mtu maalumu aliyechaguliwa na Mungu anayeshikilia ufunguo kwa ajili ya ndoto ambayo Mungu amekupatia? Kwa maombi bainisha mtu huyo anaweza kuwa ni nani. Mtafute Mungu kwa ajili ya miadi na mtu huyo katika njia ambayo inaweza kumpatia utukufu wa mwingi zaidi.

4. Soma Nehemia 2:1–8. Mfalme alipomwuliza Nehemia alichohitaji ili kujenga upya kuta zilizobomoka za Yerusalemu, Nehemia hakushtukizwa. Alikuwa na mpango aliopewa na Mungu. Je,umeandika tamko la utume ambao Mungu ameuweka moyoni mwako pamoja na kile ambacho unatakiwa kukifanya, jumlisha muda ambao utautumia kuutekeleza mpango huo? Andika ndoto au utume ambao Mungu ameweka katika moyo wako upande mmoja wa ukurasa mmoja. Shughulikia mambo yafuatayo: Hitaji ni nini? Utume wa kushughulikia wa hitaji ni nini? Ni kwa jinsi gani na ni lini utatimiza utume huo? Manufaa ya utume yanayokusudiwa ni nini? Unahitaji nini ili kutimiza utume huo? Ni uwajibikaji gani uliouweka ili kutimiza utume huu?
5. Soma tena Nehemia 2:1–8. Nehemia hakuishia tu kuomba ili Mungu ampe miadi ya Kimungu na mfalme. Alishiriki ndoto na utume mara tu Mungu alipomsukuma kuongea juu ya mpango huo! Je, umeshiriki njozi hii na watu muhimu ambao Mungu anakuletea mawazoni? Shiriki ndoto na utume huu na wale ambao Mungu anawaweka mawazoni mwako.

## Hatua za Kujua Mapenzi ya Mungu kwa Ajili ya Maisha Yako

1. Mathayo 28:18, Waefeso 1:20-22, Waefeso 6:10-12,18. Omba kwa jina lenye mamlaka la Yesu amzuie Shetani asikuchanganye au kukupotosha ili usigundue mapenzi ya Mungu.

2. Mathayo 28:18, Wafilipi 2:9-11. Salimisha ndoto zako, mazingira yako, na maisha yako kwa mamlaka ya Yesu Kristo. Tubia jambo lolote linalokufanya ukose uaminifu kwa Kristo. Tafuta kile ambacho kitampa Yesu Kristo utukufu wa juu kabisa!
3. Yakobo 1:5-8. Mwombe Mungu hekima. Amina amekupatia hekima. Usiwe na shaka.
4. Zaburi 25:5, 46:10, Yeremia 33:3. Subiri katika uwepo wa Mungu ili akufunulie hekima Yake. Subiri kwa matarajio kuwa Mungu atafunua mapenzi Yake kwako.
5. Isaya 8:20. Pima mahitimisho yako kwa Neno la Mungu lililoandikwa. Mwulize Mungu, "Je, kuna jambo lolote katika Neno Lako linalothibitisha au kukosoa majumuisho yangu?"

"Tunahitaji kufuata kwa karibu zaidi mpango wa Mungu kwa ajili ya maisha yangu. Kufanya kila tuwezalo katika kazi iliyo karibu yetu, kusalimisha njia zetu kwa Mungu, na kutazama viashiria vya uongozi Wake—hizi ndizo kanuni zinazohakikisha uongozi salama katika uchaguzi wa kazi [au huduma]. Yeye aliyetoka mbinguni awe mfano wetu alitumia takribani miaka thelathini ya maisha yake katika kazi ya kawaida, kazi ya ufundi; lakini katika kipindi hiki alikuwa akijifunza Neno na kazi za Mungu, na akisaidia, akifundisha, wote ambao mvuto Wake uliweza kuwafikia. Wakati huduma Yake ya hadhara ilipoanza, alizungumza kila mahali akiponya wagonjwa, akiwafariji wenye huzuni, na akihubiri injili kwa maskini. Hii ni kazi ya waafuasi Wake wote" (Education, uk. 267).

Kiambatanisho 5

# Vidokezo kwa Ajili ya Tabia Njema za Kidijitali

"Mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu" (Waefeso 5:16).

- Tumia kauli mbiu hii: Neno kabla ya ulimwengu!
- Salimisha simu yako kwa kwa Yesu kila asubuhi na asubuhi zote!
- Kumbuka, simu yako ni kwa ajili ya raha yako, siyo kwa ajili ya raha kila mtu mwingine yeyote.
- Fanya uchaguzi wa makusudi kutazama juu na dumu kutazama juu!
    - Tazama juu kwa Yesu kila asubuhi (Zaburi 5:3).
    - Watazame watu machoni unapoongea nao.
    - Angalia uumbaji wa asili na uzuri ambao Mungu ameuweka.
    - Fikiria jinsi unavyoweza kumbariki mtu fulani mwenye uhitaji.
- Weka simu yako katika hali ya kimya.
- Zima vitufe vya matangazo visivyokuwa vya lazima kwenye simu yako.
- Futa programu tumishi zilizokwisha muda wake, zisizokuwa za lazima, au zinazopoteza muda.
- Usiku, weka simu yako nje ya chumba chako.
- Ikiwa ni lazima utumie kengele ya kukuamsha, tumia kengele ya saa halisi, siyo kengele ya simu yako.
- Linda ibada zako za asubuhi na mifumo ya usingizi wako wa usiku kwa kutumia nyenzo za simu yako ili kuzima matangazo yote.
- Kabla ya kwenda kitandani, uwe na ibada ya familia au rafiki, kusoma kitabu, au kufurahia uumbaji badala ya kutembelea simu.
- Wakati wa asubuhi, baada ya kuwa na muda na Mungu, kwa maombi mengi panga ajenda ya siku kabla ya kuangalia jumbe kwenye simu yako au kabla ya kuvutwa na mambo mengine.

- Jibu barua pepe ambazo siyo za lazima kwa kutumia kompyuta kuliko kutumia simu yako mara moja.
- Ukiwa kazini, fanya kazi kwa saa moja au saa mbili kwa wakati mmoja simu yako ikiwa imezimwa. Utakuwa mzalishaji mzuri zaidi.
- Futa akaunti za mitandao ya kijamii kutoka katika simu yako ili usije ukajaribiwa kupoteza muda kwa kuzitembelea unapokuwa umechoka.
- Ikiwa itahitajika, tumia programu tumishi zenye vizuizi, jambo ambalo litakusaidia kupunguza muda unaotumia kutembelea mitandao ya kijamii bila kujitambua.
- Unapokula au unapotumia muda wa kutosha ukiwa na familia au marafiki, weka mbali simu mahali macho yako yasipoweza kuiona na iwe katika hali ya ukimya ili usisumbuliwe.
- Waalike wanafamilia na marafiki wa karibu wakupe mrejesho juu ya tabia zako za matumizi ya vifaa vya kidijitali, wakusaidie uelewe hali yako ya kuzidiwa na matumizi ya simu.
- Ukiwa kanisani, acha simu yako katika gari au izime kabisa.
- Fikiria kupanga nyakati za kimkakati katika maisha yako ili kuondoa sumu za kidijitali na kurekebisha vipaumbele vyako. Hilo linaweza kumaanisha kuwenda mbali na simu yako kwa siku kadhaa kwa kwa wakati mmoja au kufunga kuhusiana na masuala ya kidijitali kila Sabato. Inaweza pia kumaanisha kufunga kutumia simu kwa wiki nzima au kutumia simu isiyokuwa na mtandao wa intaneti na masuala ya mitandao ya kijamii au usumbufu wa mitandao.
- Ikiwa una mashaka kuhusiana na kitu chochote unachokisoma, unachokitazama, au unachokisikiliza, fikiria Wafilipi 4:8 kama kanuni salama ya uongozi.
- Juu ya yoyote, usiruhusu simu yako kuwa bwana wako. Kumbuka ni nani aliye Bwana wako!

Orodha iliyopo hapo juu, pamoja na nyongeza chache, imechukuliwa kutoka katika kitabu kiitwacho Daring to Live by Every Word: Loving God with Heart, Body, Mind and Soul, kilichoandikwa na Melody Mason, u.k. 161–163.

Kiambatanisho 6

# Vidokezo kwa Ajili ya Kukuza Wanafunzi Wenye Afya

"Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu" (1 Kor. 10:31).

Ili kusaidia kuzingatia kanuni kutoka Kurudi Madhabahuni kwa kina zaidi, tumejumuisha vidokezo vya kukuza mwili wenye afya njema.

> Uhusiano uliopo kati ya akili na mwili ni wa karibu sana: ikiwa kimojawapo kikiathirika, kingine kinaguswa kwa namna moja au nyingine. Ni jambo lisilowezekana kwa wanadamu, ambao wako chini ya nguvu ya tabia za dhambi, zinazodhuru afya, kuuelewa maneno matakatifu ya ukweli. Wakati akili inapokuwa imegubikwa kwa mawingu, nguvu za kimaadili hudhoofishwa, na dhambi haionekani kuwa dhambi. Mada nzuri sana, na zenye utukufu za Neno la Mungu huonekana kama hadithi zisizokuwa na faida. Shetani anaweza, kwa urahisi kabisa, kunyakua mbegu njema ambayo imepandwa katika moyo; kwa kuwa roho ipo katika hali ya kujua au kuelewa thamani yake ya kweli. Ni kwa njia hiyo ambapo tabia mbaya za uchoyo, zinazoharibu afya zinapingana na mvuto wa ujumbe unaowaandaa watu kwa ajili ya siku kuu ya Mungu (Review & Herald, November 12, 1901, par. 7).

Vidokezo vya mtindo wa maisha wa kiafya vinavyofuata vinaunganishwa na kanuni tulizozieleza katika somo hili. Unaweza kuongeza vidokezo hivyo katika changamoto za kwenda nazo nyumbani. Ni kanuni za msingi za afya zimeelezwa hapa. Mwombe Roho Mtakatifu akupe hekima ya jinsi ya kushiriki kanuni katika njia za kiubunifu, zinazovutia ambazo hata zinagusa shauku ya watoto.

Kanuni 1: Njoo kwa Yesu kama ulivyo.
Kidokezo cha Afya 1: Pata pumziko lako.

- Pata saa nane za usingizi wakati wa usiku ikiwezekana.

- Usingizi unaoupata kabla ya saa sita usiku una manufaa zaidi.
- Tumia muda katika siku nzima kutulia, kupumuzika, na kujinyoosha.
- Pumzika katika Yesu, bila kujali mazingira yako.

"Wao wamngojeao Bwana watapata nguvu mpya …" (Isaya 40:31).

> "Nafsi inayotulia kikamilifu katika Kristo ndiyo inayokuwa na bidii ya hali ya juu na utendaji mkubwa kabisa katika kazi Yake" (Steps to Christ, uk. 71).

Kanuni 2: Mheshimu Yesu kama Bwana.
Kidokezo cha Afya 2: Uwe na Kiasi.

- Salimisha mtindo wako wa maisha na tabia zako za kiafya kwa Yesu.
- Jizoeze kuwa na wastani na kiasi katika mambo yote mema na kukataa vitu vyote vyenye madhara.
- Salimisha uraibu wa aina yo yote kwa Yesu.
- Salimisha uchungu na kutokuweza kusamehe kwa Yesu.

Kanuni 3: Mgundue Yesu katika Neno na katika Maombi.
Kidokezo cha Kiafya 3: Pata mlo mzuri na hewa safi.

- Kula vyakula vyenye lishe za aina mbalimbali, mlo kamili, vyakula vya mimea (matunda, mboga za majazi, vyakula vya jamii ya karanga, mbegu, jamii ya mikunde, na nafaka isiyokobolewa).
- Kanuni kuu ya kufuata—Chakula cha asubuhi kama mfalme, chakula cha mwana wa mfalme, chakula cha usiku kama mtu maskini (ikiwa unakula usiku).
- Epuka kula kupita kiasi na kula kidogo sana.
- Epuka kula muda mfupi kabla ya kwenda kitandani kulala.
- Pumua kwa nguvu na pata hewa nyingi safi.
- Inapowezekana, fungua madirisha katika nyumba yako ili kuingiza hewa safi.
- Neno la Mungu ni mkate wetu wa kiroho, na maombi ni pumzi ya roho—usipuuze kula na kupumua!

> "Kama vile wazazi wetu wa kwanza walivyopoteza

> Edeni kwa kuendekeza uchu wa chakula, tumaini letu pekee la kuipata tena Edeni ni kwa njia ya kujikana nafsi na kudhibiti uchu wa chakula na tamaa za mwili. Nguvu inayotawala uchu wa chakula ni maangamizi ya maelfu ya watu, wakati, ikiwa wangeshinda katika kipengele hiki, ndipo wangekuwa na nguvu ya kimaadili ya kupata ushindi juu ya majaribu mengine ya Shetani" (Testimonies for the Church, vol. 3, uk. 491).

Kanuni 4: Pokea ubatizo mpya wa Roho Mtakatifu kila siku.
Kidokezo cha Afya 4: Kunywa maji ya kutosha kila siku.

- Kunywa vikombe 8–10 vya maji kila siku. (Kwa jumla, mtu mzima wa wastani anapaswa kujaribu kunywa angalau nusu ya aunsi kwa kila paundi moja ya uzito wake. Kwa mfano, ikiwa una uzito wa paundi 150, unapaswa kunywa takribani aunsi 75 za maji kwa siku. Kuna aunsi 8 katika kikombe, ili iwe vikombe 9 vya maji kwa siku, au lita 2.2 kwa siku)
- Beba chupa ya maji kila unapokwenda ili ikukumbushe kunywa maji.
- Epuka soda na vinywaji baridi, vinavyokausha mwili.
- Kunywa maji kabla ya kuhisi kiu.
- Oga kila siku na jizoeze usafi
- Tumia tiba ya maji kulingana na mahitaji kuongeza kinga ya mwili (kuoga maji ya moto ya baridi, n.k.).
- Kunya kinywaji kinachosafisha mwili na omba kwa ajili ya nguvu ya Roho Mtakatifu akufunulie mambo yanayohitajika kusafishwa katika roho.

Kanuni 5: Ipende familia yako kwa kujitoa mhanga.
Kidokezo cha Kiafya 5: Furahia mwanga wa jua.

- Amka na mwanga wa jua.
- Tumia angalau dakika 10–20 ukiwa katika mwanga wa jua, asubuhi na jioni.
- Epuka kuchomwa na jua.
- Uwe mwanga wa jua kwa familia yako na wale unaowapenda, ukiakisi upendo wa Yesu kila mahali unapokwenda.

Kanuni 6: Wafanye wengine kuwa wanafunzi wa Yesu.
Kidokezo cha Kiafya 6: Dumu kuughulisha kimwili.

- Lenga kufanya mazoezi kwa muda wa dakika 30–60 kila siku.
- Ujishughulishe siku nzima.
- Pitia katika ngazi kuliko kutumia lifti.
- Ishi Neno la Mungu kila siku.
- Dumu kujishughulisha kushiriki imani yako na kuwafanya wengine kuwa wanafunzi.

Kanuni 7: Fuata utume uliopewa na Mungu.
Kidokezo cha Kiafya 7: Mtumaini Mungu!

- Mtumaini Mungu kwa kusalimisha maisha yako kwa Mungu—kikamilifu, kabisa!
- Mtumainie Mungu hata kwa maswali ya maisha yasiyojibiwa.
- Mpe Mungu moyo wako na mapenzi yako kila siku.
- Kaa ndani Yake na Mwombe akae ndani yako.
- Ishi kwa ajili ya utukufu wa Wake!

“Basi, mlapo, au mnywapo, au mtendapo neno lo lote, fanyeni yote kwa utukufu wa Mungu (1 Kor. 10:31).

Kiambatanisho 7

# Funguo za Kupata Uzoefu wa Neno la Mungu

Pengine unajiuliza ni jinsi gani unaweza kuweka kumbukumbu na kuzama zaidi katika Neno la Mungu? Tunatumaini kuwa vidokezo vifuatavyo vitakusaidia.

- Kwa maombi mengi fungua Neno la Mungu ukiwa na moyo unaofundishika.
- Soma sehemu ya maandiko ya Biblia mara kadhaa, ukiruhusu Maandiko yajitafsiri yenyewe.
- Zungushia na pigia mstari maneno, mada, au vifungu vya maneno yenye uzito.
- Pigia mstari ahadi na maneno yanayotia moyo.
- Tafakari juu ya sehemu za Maandiko na aya zinazoongea na wewe.
- Uliza maswali kama:
    - Sehemu hii ya Maandiko ina ujumbe gani?
    - Muktadha unaozunguka sehemu hii ya Maandiko in upi?
    - Mungu anaongea nini na mimi katika sehemu hii ya Maandiko?
    - Ni amri zipi, mafundisho gani, na kanuni gani za maisha zinapatikana hapa?
    - Ni mabadiliko gani napaswa kumwomba Mungu niyafanye ili niende sawasa na Andiko hili?
    - Ninajifunza nini kuhusu tabia ya Mungu katika sehemu hii ya Maandiko?
    - Ni kwa jinsi gani Andiko hili linanionesha picha mpya ya Yesu?
    - Kwa jinsi gani Pambano Kuu limeoneshwa katika sehemu hii ya Maandiko?
- Omba sehemu ya Maandiko aya kwa aya, ukiifanya kuwa sehemu ya maisha yako binafsi.
- Unapoomba, sikiliza kile ambacho Roho Mtakatifu anakuonesha.
- Weka kumbukumbu ya mawazo ya kiroho ambayo Mungu anakupatia.
- Weka kumbukumbu ya ombi la ibada, ikiwa ni pamoja na sifa, ungamo, shukurani, na kujisalimisha kwa Mungu kama matokeo yake.

- Andika mambo yako maalumu ya kuombea, ukiambatanisha na ahadi za Biblia kwa maombi hayo. Andika majibu yoyote unayoyapokea kwa maombi hayo.
- Andika kumbukumbu ya wazo la muhtasari kutokana na muda wako pamoja na Mungu ambayo ungeshiriki na mtu mwingine leo.

<u>Mawazo ya Nyongeza kwa Ajili ya Kukuza Ujifunzaji wa ko wa Biblia</u>

- Uliza maswali ya "Nani, Nini, Lini, Wapi, Kwa Nini, Kwa Jinsi Gani."
- Soma sehemu ya maandiko ya Biblia katika tafsiri mbalimbali za Biblia.
- Angali aya zingine zinazorejelea aya hiyo na sehemu za Maandiko zilizo sababa hiyo sehemu ya Maanidiko unayoichunguza.
- Angalia maneno ya msingi katika Kigriki na Kiebrania au tumia Biblia ya Kujifunzia inayofafanua maneno hayo ya msingi.
- Read Ellen G. White's comments on the passage.
- Soma fafanuzi zingine za Biblia zinazoaminika.

> "Maneno yako yalionekana, nami nikayala; na maneno yako yalikuwa ni furaha kwangu, na shangwe ya moyo wangu." (Yer. 15:16)
>
> "Ishi madhabahuni. Imarisha makusudi yako kwa ahadi za Mungu" (Testimonies to the Church, vol. 1, uk. 169).

# Zana za Uanafunzi na Kurudi Madhabahuni

Mpango wa Kurudi Madhabahuni unahusu kusaidia kanisa la Mungu ligundue mahali pa kila siku kwa ajili ya Mungu katika kila moyo na kila nyumba. Kwa maelezo zaidi tembelea: www.backtothealtar.org

Je, unatafuta vitendea kazi vya nyongeza kama kijitabu hiki?

Tembelea indiscipleship.org kwa ajili ya vitabu na masomo yaliyoandaliwa na Don MacLafferty ya kupakua bure. Mafundisho haya yote yanaweza kutumiwa kwa ajili ya ukuaji binafsi na/au kwa ajili ya vikundi vidogo vidogo.

- Inside Out – Kinachoziita familia kuwekeza kwa Mungu na kuwafanya watoto wao kuwa wanafunzi.
- Come Home – Mafundisho ya vikundi vidogo vidogo ya kuwaita watu na wanandoa kurudi madhabahuni, ili kuishi njozi ya Mungu kwa ajili ya nyumbani katika kujiandaa kwa ajili ya ujio ulio karibu wa Kristo.
- Meet Jesus Outside: Bible Prayer Walks – Matembezi ya nje ya nyumba kwa ajili ya watoto, vijana,  na watu wazima wapate uzoefu na Mungu katika Neno Lake, katika Kitbau Chake cha uumbaji, maombi, na matendo.
- Jesus' Last Love Letter: A Revival for Children, Youth, and Adults – Notisi za mwalimu kwa ajili ya mikutano saba ya majadiliano, na mahusiano ya vizazi tofauti,  kinawaita wote kuja kwa Yesu kama Rafiki, Mwokozi na Bwana.
- Follow – Mafundisho ya Biblia ya hatua kwa hatua ya kutumia katika kumfanya mtu kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo. Yanaweza kutumiwa kwa ajili ya mtu na mtu au katika vikundi vidogo vidogo.
- Discipling the New Generations – Masomo ya vikundi vidogo vidogo kwa ajili ya wazazi / walezi/ wanafunzi kwa ajili ya kukuza wanafunzi wa Yesu wanaojua na wanaoishi kweli zinazobadilisha maisha kwa njia ya nguvu ya Roho Mtakafitu.

- Live Like Elijah – Visa vinavyobadili maisha kutoka katika safari binafsi ya familia ya MacLafferty ya kuishi kwa imani. Yamejumuishwa pia masomo ya kukusaidia wewe kugundua kusudi na jinsi ya kuishi kila siku ukiwa na uaminifu usiokuwa na hofu, ukipumzika katika uongozi na uwezeshaji wa Mungu.

Vitendea Kazi na Zana za Nyongeza za Ibada

Kutoka Huduma za Familia GC

- Rebuilding the Family Altar – https://family.adventist.org/resources/rtfa/
- Fun and Easy Family Worship Memories – https://family.adventist.org/resources/fun- easy-family-worship-memories/

Kutoka Huduma za Vijana GC

- Developing an Authentic Devotional Life – https://bit.ly/GCyouthministries1
- Morning Watch: In the Word for Youth – https://www.gcyouthministries.org/resources/m orning-watch/

Kutoka Huduma za Watoto GC

- Bible Studies for Young Readers – https://www.faithfinders.com/bible-studies
- Back to the Altar: 10 Days of Prayer for Children – https://www.faithfinders.com/ten-days-of-prayer-2023.pdf

Tembelea revivalandreformation.org kwa ajili ya mamia ya zana zenye msaada za ziada na vitendea kazi vya bure kukuza utembeaji wako na Yesu kwa njia ya kujifunza Biblia, maombi, ibada, na ushuhuda.

Unatafuta msaada kwa ajili ya kutegemezwa kwa maombi? Jiunge na familia ya kanisa la ulimwengu wakati wowote, mchana au usiku, katika maombi yetu ya Zoom ya saa 24/7 ita hapa 247unitedprayer.org. Ungana na wengine wanaoomba kwa ajili ya Mvua ya Masika.

MWONGOZO WA “KURUDI MADHABAHUNI” ULIOTOLEWA NA KONFERENSI KUU

KITABU HIKI HAKIUZWI